



Ripoti ya Kamati Maalum ya Kuhakiki Ukosefu wa Usawa
wa Kihistoria katika kumbukumbu za Maadhimisho

Mwenyekiti wa kamati

Bwana Tim Hitchens KCVO CMG

Imefanyiwa utafiti, Imekusanywa na kuandikwa na

Dkt George Hay

Dkt John Burke

Wanakamati

Profesa Michèle Barrett

Shrabani Basu

Selena Carty

Blondel Cluff CBE

Profesa Mark Connelly

Terry Denham

Amandeep Madra OBE

Edward Paice

Trevor Phillips OBE

Dkt Gavin Rand

Dkt Anne Samson

Dkt Kevin Searle

Dkt Daniel Steinbach

Dkt Nicholas Westcott CMG

Mnamo Desemba 2019, Makamishna wa Tume ya Makaburi ya Vita ya Jumuiya ya Madola (CWGC) walichagua kuteua kamati ya wataalam huru na wawakilishi wa jamii ili kufanya yafuatayo:

- Kuchambua vitendo vya kihistoria vya CWGC katika muktadha wa ulimwengu ili kutambua na, kila inapowezekana, kurekebisha mapungufu yoyote katika kumbukumbu za maadhimisho.
- Kutoa mapendekezo ambayo yatasaidia kuunda kazi za baadaye za CWGC.

Wakati wa kuanzishwa, ilifikiriwa kuwa Kamati hiyo ingekutana uso kwa uso katika Makao Makuu ya CWGC huko Maidenhead, ikimaanisha uwakilishi ulikuwa Uingereza. Kamati ilitakiwa isiwe na upendeleo, yenye malengo hakika na kutoa ripoti ya ukweli, hata kama yataleta wasiwasi. Bwana Tim Hitchens, Kamishna wa CWGC, aliteuliwa kama Mwenyekiti wa Kamati Maalum.

Yaliyomo

1. Muhtasari wa Utendaji

2. Utangulizi

- i. Hatari za ridhaa
- ii. Ujumbe juu ya mbinu, upeo na mapungufu
- iii. Istilahi na lugha

3. Sehemu ya 1 - Vita vya himaya na watu wa himaya

- i. Kuajiri, huduma na kutambuliwa
- ii. Kuelezea shida

4. Sehemu 2 - Majukumu na wajibu wa IWGC

- i. Uanzishwaji, kanuni na umuhimu wa Medani ya Mapambano ya Magharibi
- ii. Mirathi ya mazishi wakati wa vita, usajili wa makaburi na ubaguzi katika maandishi

5. Sehemu 3 - Makosa, uangalizi na dhuluma

- i. Mmenyuko badala ya hatua
- ii. Mipaka ya usawa
- iii. Uainishaji na mifano

6. Sehemu 4 - Muhtasari na mapendekezo

- i. Hitimisho
- ii. Mapendekezo

7. Viambatisho

- i. Kiambatisho 1 - Majedwali ya kupima ukosefu wa usawa katika kumbukumbu
- ii. Kiambatisho 2 - Wahusika wa kamati na wasifu
- iii. Kiambatisho 3 - Bibliografia iliyochaguliwa

Muhtasari wa Utendaji

Kamati hii Maalum ilitiuliwa kuchunguza historia ya awali ya Tume ya Makaburi ya Vita vya Himaya (IWGC) ili kubaini ukosefu wa usawa katika jinsi shirika lilivyokumbuka wafu wa Dola ya Uingereza katika vita viwili vya dunia. Pale ambapo ukosefu wa usawa huo uligunduliwa, ilitakiwa kutoa mapendekezo kadhaa ambayo yangeweza kusaidia na kuongoza Tume ya Makaburi ya Vita vya Jumuiya ya Madola ya sasa (CWGC) katika kuyajibu. Kutokana na shida zinazosababishwa na janga la Uviko COVID-19 (UVIKO) na ukubwa wa kazi mara tu itakapoanza, Kamati iliwekea umakini wake katika shughuli za IWGC wakati na baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia.

Ilianzishwa zaidi ya karne moja iliyopita kuadhimisha vifo vilivyotokana na Vita vya Kwanza vya Dunia katika Dola la Uingereza, tangu mwanzoni kazi ya IWGC ilifanuliwa na kanuni ya usawa katika kifo. Bila ya kujali cheo cha mtu binafsi katika maisha ya kijamii au ya kijeshi, bila ya kujali dini yake, wangepadhimishwa sawasawa - na jina lao likiwa limechorwa ama kwenye jiwe la juu ya kaburi lililotambulika au kwenye kumbukumbu ya waliopotea. Ingawa kanuni hiyo ilikuwa ya kupendeza, na Ulaya ilifanikiwa vyema, ripoti hii imegundua kuwa ahadi ya usawa ilikuwa na mipaka mahali pengine.

Ikikinzana na kanuni za uanzishaji wa shirika, inakadiriwa kuwa kati ya majeruhi 45,000 na 54,000 (wengi wao wakiwa ni Wahindi, Afrika Mashariki, Afrika Magharibi, Wamisri na Wasomali) waliadhimishwa bila usawa. Kwa wengine, badala ya kuweka alama kwenye makaburi binafsi, kama IWGC ingefanya Ulaya, wanaume hawa walikumbukwa kwa pamoja kwenye kumbukumbu. Kwa wengine ambao walipotea, majina yao yalirekodiwa katika rejista badala ya kurekodiwa katika jiwe.

Majeruhi wengine 116,000 (haswa, lakini sio peke yao, wafanyakazi wa Afrika Mashariki na Wamisri) - lakini wanaoweza kufikia idadi ya 350,000 - hawakuadhimishwa kwa jina au labda hawakuadhimishwa kabisa. Wengi kati ya wanaume hawa waliadhimishwa na kumbukumbu ambazo hazikuwa na majina yao - kwa upande mmoja ni kwa sababu IWGC haikupewa majina yao au mamlaka ya kijeshi au ya kikoloni haikuwapa mahali pao pa kuzikwa, na upande mwingine ni kwa sababu ya uamuzi wa kutofuata kanuni zake kwa

imani kwamba jamii ambazo wanaume hawa walitoka hazingeweza kutambua au kuthamini aina kama hizi za kuadhimisha.

Ripoti hii imegundua kuwa katika miaka ya 1920, kote Afrika, Mashariki ya Kati na India, itikadi ya kifalme iliathiri utendaji wa IWGC kwa njia ambayo haikufanya huko Ulaya, na sheria na kanuni ambazo zilikuwa takatifu huko hazikuzingatiwa kila wakati mahali pengine. Matokeo yake ni kwamba, mitazamo ya kisasa juu ya imani zisizo za Ulaya na ibada tofauti za mazishi, na hali ya mtu binafsi au kikundi inavyoonekana kama "hali ya kistaarabu", iliathiri maadhimisho katika kifo.

Ingawa katika idadi kubwa ya kesi IWGC haikuchukua uamuzi wa kutofuata kanuni zake kwa umoja, inapaswa kuzingatiwa kuwa inahusika katika zote. Ingawa hatupaswi kusahau kazi ya Tume iliyokuwa na mafanikio na iliyojumuisha wengi Ulaya na kwingineko ulimwenguni, pia hatupaswi kupuuza makosa katika historia ya awali ya shirika - makosa mengi ambayo yamesahaulika au kufikirika upya katika zaidi ya karne ya uwepo wake.

Ili CWGC ijishughulishe vyema na historia hii na kuchukua hatua katika kusahihisha na kuelezea makosa ya zamani, Kamati hii inatoa mapendekezo kumi kulingana na mada kuu tatu:

- Kupanuliwa kwa utafutaji wa kijiografia na kihistoria katika rekodi ya kihistoria ya ukosefu wa usawa katika ukumbusho na kufanyia kazi kile kitakachopatikana.
- Kufanya upya ahadi ya usawa katika kuadhimisha kwa kupitia ujenzi wa miundo ya kumbukumbu ya kimaumbile au ya kidijitali.
- Kutambuliwa na kukubalika kwa historia hii ngumu na kuishirikisha na jamii zote za Dola ya zamani ya Uingereza ambayo iliguswa na vita viwili vya dunia.

Utangulizi

i. Hatari za ridhaa

Tume ya Makaburi ya Vita vya Himaya (IWGC) ilianzishwa mnamo 1917 kuadhimisha kumbukumbu za milele za wanaume na wanawake wa Dola la Uingereza waliopoteza maisha yao katika Vita vya Kwanza vya Dunia. Ikapanua mkataba wake kuingiza mzozo mwingine mmoja tu, Vita vya Pili vya Dunia, na sasa - zaidi ya karne moja tangu ianzishwe - inahifadhi kumbukumbu ya zaidi ya raia milioni 1.7 wa Jumuiya ya Madola waliokufa katika mapambano hayo.¹ Inafanya hivyo kwa kutunza makaburi na ukumbusho katika zaidi ya sehemu 23,000 kote ulimwenguni, wakati pia ikitoa hifadhidata ya mtandaoni inayosimamiwa na majina na maelezo ya wale walio katika utunzaji wake.

Mkataba wa Kifalme na ripoti kadhaa za maelezo ya muundo ziliunda njia ambayo IWGC ilifanya kazi baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia na, hivi karibuni, jinsi Tume ya Makaburi ya Vita vya Jumuiya ya Madola (CWGC) ilivyoangazia kazi hiyo.² Wazo hili, lililosukumwa zaidi na idhimisho la miaka mia moja ya uwepo wa shirika mnamo 2017, limetoa taarifa kwa umma kuhusu maadili na kanuni zake za uanzilishi, ambazo ziligawanywa katika kauli kuu nne:

- Kila mmoja ya wafu wa Jumuiya ya Madola anapaswa kukumbukwa kwa jina kwenye jiwe la kaburi au kuadhimishwa.
- Mawe ya makaburi na maadhimisho yadumu milele.
- Mawe ya makaburi yawe sare.

¹ Ili kukubalika katika maadhimisho kama mjeruhiwa wa Vita vya Kwanza vya Dunia, wafanyikazi wa huduma wanatakiwa wawe wamefariki kati ya tarehe 4 Agosti 1914 (Siku ya Tamko kuu la Uingereza la Vita) na 31 Agosti 1921 (mwisho rasmi wa vita kufuatia Agizo la Baraza lililohitajika ili Kusitishwa kutokana na (Ufafanuzi) wa Sheria ya Vita ya Sasa. Kwa Vita vya Pili vya Dunia tarehe ni 3 Septemba 1939 (Tamko kuu la Uingereza juu ya vita) na 31 Desemba 1947 (tarehe iliyokubaliwa na serikali zilizoshiriki ili kuwepo na kipindi cha baada ya vita karibu sawa na kile cha Vita vya Kwanza vya Dunia). Kifo baada ya kuachishwa bado kinakubalika kama ni mjeruhi anayestahili maadhimisho kama kinahusika moja kwa moja na huduma vitani.

² Katika kutambua mahusiano yaliyobadilika kati ya Uingereza na tawala na koloni zake za zamani, lakini pia ikiwa na uhakika wa umuhimu wa kazi yake, shirika lilibadili jina kwa kutoa neno 'Himaya' na kuweka 'Jumuiya ya Madola' tangu Machi 1960.

- Kuwepo usawa kati ya wafu wa vita bila ya kujali cheo au dini.³

Ilikuwa moja ya ripoti za maelezo zilizotajwa ambazo zilitoa asili ya kanuni hizi. Hii ilikamilishwa kwa Tume katika msimu wa vuli wa 1918 na Luteni-Kanali Bwana Frederic Kenyon - Mkurugenzi wa Jumba la Makumbusho la Uingereza na Mkurugenzi wa Sanaa kwa IWGC - baada ya kushauriana na jamaa za wafu, vikosi vya jeshi, viongozi wa dini na wawakilishi wa sanaa. Hapa ilitamkwa kwamba "wote, bila kujali vyeo vyao vya kijeshi au nafasi yao katika maisha, wanapaswa kuwa sawa katika makaburi yao" na, labda muhimu zaidi, "kwamba heshima isipungue katika sehemu za mapumziko ya mwisho ya Wahindi na wanachama wengine wa Himaya ambao si Wakristo kama isivyopungua kwa askari wetu wa Uingereza".⁴

Ukijumlisha heshima na uzuri wa maeneo ya kumbukumbu kama Neuve Chapelle huko Ufaransa ambayo ipo kwa ajili ya vikosi vya India kabla ya nchi hiyo kugawanywa, au makaburi ya amani ambayo yapo kwenye nchi zilizokuwa mstari wa mbele kote ulimwenguni, inaonekana kuwa hakuna tofauti kati ya wale waliozikwa, kijuujuu, kuna machache yanayoweza kuonyesha kwamba Tume imefanya chochote isipokuwa kuzingatia maadili haya. Walakini, tangu kazi zake kuu kukamilishwa, tofauti kadhaa za kihistoria katika ukumbusho zimetambuliwa na shirika, na marekebisho na nyongeza zimefanywa, zinaendelea kufanywa au zimepangwa kufanywa kwa maeneo kadhaa ulimwenguni.⁵ Hata hivyo, hadi sasa, swali la jinsi tofauti zilivyojitokeza, pamoja na suala kubwa la kutoadhimisha au kutokuwepo usawa kati ya majeruhi halijawahi kuchunguzwa kikamilifu na CWGC. Hivyo hivyo, ingawa iligundua na kusahihisha maswala mengi, shirika halikubadilisha maelezo yake ya asili ili kuingiza na kuelezea makosa haya ya kihistoria na jinsi ambavyo zilikiuka kanuni zao wenyewe za ulimwengu ambazo hutajwa mara nyingi.

³ Kanuni hizi zimekuwepo katika matamko tofauti ya tovuti ya CWGC tangu angalau 1998. Matamko haya yaliwekwa kinagaubaga ndani ya Ripoti ya Mwaka ya Hamsini na Mbili mnamo 1970 -71, p. 3.

⁴ Kenyon, Lt-Kol. Bwana Frederic, *War Graves - how the cemeteries abroad will be designed* (Makaburi ya Vita - jinsi makaburi ugenini yatakavyoundwa) (London: HMSO, 1918), pp. 7 & 11.

⁵ Tazama Jedwali A2, A3 na A5 katika Kiambatisho 1 kwa orodha kamili ya maeneo haya.

Ingawa uhakiki wa hali hii ulicheleweshwa, kichocheo cha kuundwa kwa Kamati hii na uchunguzi wake ilikuwa programu ya saa moja ya televisheni ya Channel 4 iliyoitwa *Unremembered* (Wasiokumbukwa). Ilitangazwa mnamo Novemba 2019, na ilichunguza yale ambayo Tume ya Makaburi ya Vita vya Himaya iliyowafanyia Waafrika waliokufa baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Kipindi hicho kilitangazwa na mbunge David Lammy na kutolewa maelezo kutokana na utafiti wa Profesa Michèle Barrett. Kipindi hicho kiliwasilisha ushahidi ulioonyesha kwamba, katika mifano kadhaa huko Afrika Mashariki, Tume ilishindwa kutimiza maadili yake ya usawa. Kwa upande mmoja, Kamati hii iliundwa kuchunguza mifano hii lakini pia kupanua, kwa mapana, utafiti wa shida kama hizo ambazo zinaweza kuwepo mahali pengine.

Ushahidi uliorekodiwa hapa unaonyesha hatua za awali za uchunguzi wa kesi za ukosefu wa usawa wa maadhimisho na kutokuwepo maadhimisho, na jukumu la IWGC katika kuonyesha yote. Inaonyesha kuwa tofauti zinazotokana na kanuni za shirika zipo nje ya Ulaya na katika maeneo yenye mali yake, haswa zinaweza kuwekwa katika vikundi viwili:

- Kwanza, inakadiriwa kuwa kati ya majeruhi 45,000 na 54,000 wameadhimishwa au walikumbukwa kwa njia tofauti Afrika Mashariki, Afrika Magharibi, Misri na Mashariki ya Kati - kawaida kwa pamoja kupitia kumbukumbu wakati wengine wangekuwa wamewekewa alama ya mazishi, au kwa kurekodi majina ya wafu kwa kuwasajili badala ya kuchonga kwenye jiwe.
- Pili, inakadiriwa kuwa angalau majeruhi 116,000, lakini kuna uwezekano wa kuwa 350,000, hawawezi kuadhimishwa kwa jina au hawawezi kuadhimishwa kabisa, haswa Afrika Mashariki na Misri.

Maswala yote mawili ni matokeo ya maamuzi yaliyofanywa na IWGC, japo ni maamuzi yaliyoathiriwa na uhaba wa habari, makosa yaliyorithiwa kutoka katika mashirika mengine na maoni ya wasimamizi wa kikoloni. Maamuzi haya yote yanafungamana na chuki zilizokita mizizi, dhana za awali na ubaguzi wa rangi ulioenea unaohusiana na mitazamo ya kisasa katika himaya.

Kamati inakubali kuwa dhana zilizochunguzwa katika ripoti hii zina uwezekano wa kuwa na ugomvi, kupingwa na kugawanya watu, haswa wale wanaoshikamana na kabila, utamaduni, lugha, tabaka na dini, na jinsi zilivyotumiwa na wengine kujenga safu za kikabila. Walakini, hakuna shaka kwamba dhana hizi zilikuwa ni msingi wenye ukosefu wa usawa kati ya wafu nje ya Ulaya. Jambo hili halijashughulikiwa sana ndani ya ripoti hii kwani, pale ilipowezekana, rekodi yake ya sasa imeweza kujionyesha waziwazi. Wasomaji wa kisasa hawatapata shida kutafautisha mitazamo ya msingi.

Ripoti hii ni nyongeza ya kundi la maandishi yanayochunguza maswala haya, kubainisha, kuweka muktadha, kuchunguza na kutafuta uelewa wa sera na mazoea ya IWGC ya wakati huo ambayo yalisababisha ubaguzi, huku yakiainisha matokeo ya shughuli hiyo.⁶ Mapendekezo yanayofuata yamependekazwa na Kamati hii kama njia ambazo CWGC inaweza kuchukua katika hatua za kutambua, kuelewa na, inapowezekana, kurekebisha ukosefu wa haki, makosa na kupitiwa kulikotokea zamani.

ii. Ujumbe juu ya mbinu, upeo na mapungufu

Utafiti ulianza katika majira ya kuchipua ya 2020, wakati janga la COVID-19 (UVIKO) lilipoanza kuathiri maisha ya watu kuhusu kazi na pia kupunguza uwezo wa kupata nyenzo muhimu za kumbukumbu. Ingawa mradi ulikuwa umewekewa mipaka, hakukuwa na njia ya kujua kiwango cha maswala ambayo ungeweza kufichua au kufahamu upeo wa kazi. Matokeo yake ni kwamba, ilipangwa kuwa nyaraka za CWGC zitakua ndio mahali pa kuanzia kazi na timu ya utafiti itatambua viungo kwenye makusanyo mengine ambayo yangefanyiwa kazi katika awamu za baadaye. Uhalisia ni kwamba sheria kali za watu

⁶ Tazama, kwa mfano: Barrett, Michèle, 'Subalterns at War: First World War Colonial Forces and the Politics of the Imperial War Graves Commission', *Interventions*, Vol. 9, Na. 3 (2007), pp. 451–74; Barrett, Michèle, 'Afterword Death and the afterlife: Britain's colonies and dominions', in Santanu Das (ed.), *Race, Empire and First World War Writing* (Cambridge: Cambridge University Press, 2011), pp. 301–20; Barrett, Michèle, "'White Graves" and Natives: The Imperial War Graves Commission in East and West Africa, 1918–1919', in Paul Cornish and Nicholas Saunders (eds), *Bodies in Conflict: Corporeality, materiality, and transformation* (London: Routledge, 2014), pp. 195–218; Barrett, Michèle, 'Dehumanisation and the War in East Africa', *War & Culture Studies*, Vol. 10, Na. 3 (2017), pp. 238–52; Siblon, John, 'Negotiating Hierarchy and Memory: African and Caribbean Troops from Former British Colonies in London's Imperial Spaces', *The London Journal*, Vol. 41, No. 3 (2016), pp. 299–312; Siblon, John, "'Race", rank, and the politics of inter-war commemoration of African and Caribbean servicemen in Britain', in Hakim Adi (ed.), *Black British History: New Perspectives* (London: Zed Books, 2019), pp. 52–70.

kutoruhusiwa kutoka nje ya nyumba ziliambatana na mwanzo wa utafiti, ambao kwa kiasi kikubwa ulizua shughuli hii sio tu kwa makusanyo ya CWGC yenyewe lakini pia kwa nyenzo za kidijitali.

Ingawa hapo awali utafiti huu ulitakiwa kuchunguza kazi ya Tume ilivyojijusisha na majeruhi wa vita vyote vya dunia, vizuizi vilivyotajwa vililazimisha timu ya utafiti kufikiria upya wigo wake, na kusababisha mwelekeo wa makusudi kwenye Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia na kipindi cha katikati ya vita. Mafaili mengi ya nchi yanayohusu Afrika Mashariki, Afrika Magharibi na mafaili mengi ya utendaji kwa Ulaya yalikuwa tayari yamewekwa kidijitali na timu ya Hifadhi ya CWGC. Kutokana na ahadi zinazoendelea za kuufungua mkusanyiko huu na kuelewa vizuri historia yake, Tume huweka kumbukumbu za muhtasari wa matukio pamoja na nyaraka zingine husika ambazo zilipatikana. Yanayowasilishwa hapa yanatokana na shughuli za IWGC huko Ulaya, Afrika Mashariki, Afrika Magharibi na Mashariki ya Kati baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia.⁷ Kwa kuzingatia utafiti uliopo ambao umeshatajwa, ilikuwa kote Afrika ambapo idadi kubwa zaidi ya kasoro za ukumbusho zilitabiriwa kuwepo, na matokeo ya ripoti hii yanathibitisha hili. Ingawa hii ni sehemu ya matokeo ya nyenzo zilizohusishwa, pia inaonyesha maswala ya kipekee, uzoefu na maamuzi yaliyofanywa kwenye bara hilo. Walakini, inamaanisha pia kwamba matokeo ya ripoti hii yanaweza kuonekana tu kama awamu ya kwanza ya uchunguzi mpana ambao unapaswa kujumuisha maeneo yote ya kazi ya Tume iliyounganishwa na vita vyote vya dunia.

Ripoti hii ilifanyiwa utafiti, iliandaliwa na kuandikwa na Dkt George Hay na Dkt John Burke chini ya ushauri na mwongozo wa Kamati Maalum. Mapendekezo mwishoni mwa ripoti hii yalitungwa na Kamati kupitia tafakari na majadiliano na kupelekwa CWGC ili kuzingatiwa na kukubalika. Mapendekezo si maalum, yanaweza kubadilishwa na kutumiwa kwa maswala yote yaliyotabiriwa ambayo CWGC inaweza kuhitaji kushughulikia siku zijazo, bila hatari ya kurudia makosa ya zamani.

⁷ Wakati mfupi na ugumu wa kupata nyenzo za kumbukumbu huko Maidenhead kwa sababu ya vizuizi vya kusafiri inamaanisha ripoti hii ina kikomo cha uwezo wa kutafuta maswala yoyote kwa undani nchini Afrika Kusini. Hii pamoja na maeneo mengine mengi ya kijiografia na mpangilio wa nyakati, kutahitaji kuwa sehemu ya miradi ya baadaye.

Vizuizi walivyowekewa timu ya utafiti havijazuia utambuzi wa maeneo mengine ya uchunguzi katika nyaraka za Tume, au nyenzo zinazopatikana ulimwenguni ambazo zinaweza kusaidia kazi hii katika siku zijazo. Ingawa sehemu hii ya mradi haingeweza kuwa kamili katika muda uliopatikana, hata bila vizuizi juu ya harakati, imeweza kutoa mifano ya kutosha kuiruhusu Kamati hii kutoa mapendekezo sahihi. Kuna umuhimu wa kutaja mapendekezo ya kwanza hapa: kwamba CWGC inapaswa kuendelea na utafiti huu ili iweze kuelewa kwa kina kiwango cha matatizo haya na kutekeleza hatua muhimu za kurekebisha.

iii. Istilahi na lugha

Wakati wa kuandika kuhusu taasisi yoyote ya Uingereza iliyoanzishwa wakati wa ustawi wa himaya, ni muhimu kutilia maanani istilahi za kisasa na lugha, na njia ambazo zitatumika na kurudiwa katika maandishi. Nyenzo nyingi ambazo zimeweza kutoa taarifa katika ripoti hii zimetolewa kutoka kwenye kumbukumbu za taasisi kutoka miaka ya 1920, na kutoka kwenye taasisi ambayo ilitokana na himaya. Ingawa kazi yake ilisukumwa na hisia za umoja katika dhabihu ya kawaida, umoja huo ulionekana kupitia lensi ya ubeberu wa Uingereza. Kwa hivyo, inapaswa kueleweka kuwa istilahi na lugha inayotumiwa na shirika ni tofauti sana na kile tunachoamini kinakubalika mnamo 2021. Hii sio kutetea matumizi yake bali ni kusema tu kwamba ilikuwa ni zao la nyakati zake.

Moja ya jambo muhimu lililogunduliwa na ripoti hii ni kwamba sharti la IWGC la kuweka usawa katika utunzaji wa maadhimisho - na kwa hivyo usawa katika kifo - lilikuwa na mipaka ya kijiografia. Kwa askari wa vikosi vya himaya waliokufa nje ya Ulaya, lakini haswa kote Afrika, Mashariki ya Kati na India, jinsi walivyotendewa mara nyingi kulikuwa na tofauti. Wakati wa kufanya kazi katika medani hizo, IWGC iliweka wafu katika vikundi vifuatavyo: 1) wale ambao walikuwa 'weupe' (mara nyingi huitwa 'Wazungu'), Watu wa visiwa vya West Indies, watu waliochanganya rangi wa Afrika Kusini yaani waliochanganya

na Wachina; 2) Wahindi na 3) makabila mengine yote, kwa ujumla waliojulikana kama 'wenyeji'.⁸

Waandishi wamenukuu maneno katika makundi ya sasa ya IWGC pale walipozungumzia sera au vitendo ambavyo vilitegemea kunukua. Wakati wa kuzungumzia Afrika, neno 'mwenyeji' (daima katika nukuu) linaashiria Waafrika 'wasio wazungu'. Katika kuangazia matumizi ya IWGC, maana moja imetumika kwa maneno ya pamoja, kama vile wanajeshi wa Kiafrika na wafu wa Kiafrika. Hii inaweza kujumuisha makundi mengi sana ya watu wenye kabila na lugha tofauti, isipokuwa zile za asili ya kizungu za Ulaya. Kikundi hiki cha mwisho kawaida huitwa "Wazungu" katika nyaraka hii, kama vile ambavyo wangaliitwa na IWGC. Wakati wa kuweka matokeo ya sera na vitendo, waandishi wamejitahidi kutumia istilahi ambayo ni sahihi zaidi na inayofaa kwa wale walioathiriwa.

Nchi, wilaya na majina ya sehemu zitaitwa kwa kutumia majina ya awali kama ilivyokuwa wakati wa matukio yanayotajwa. Hii itafuatwa na jina linalofaa la sasa ambalo litawekwa kwenye mabano.

⁸ Wachina wanaotajwa hapa ni wale wa Kikosi cha Wafanyakazi cha Kichina waliofanya kazi pande za Magharibi. Hapa IWGC iliweka alama ya makaburi na zaidi ya hapo walitambua na kuzingatia ibada zinazofaa za mazishi. Hata hivyo, hii haikuwa kwa majeruhi wote wa China, kwani wale waliopotea na Jeshi la India, katika medani nyingine au waliopotea baharini walikumbukwa kwenye Uadhimisho wa Hong Kong, ambao kabla ya 2006 haukuwa na majina yao.

SEHEMU YA 1 - VITA VYA HIMAYA NA WATU WA HIMAYA

i. Kuajiri, huduma na kutambuliwa

Ushindi katika Vita vya Kwanza vya Dunia uligharimu Uingereza zaidi ya maisha 800,000.⁹ Makoloni na Utawala wa Himaya kubwa ya Uingereza pia ililipa bei kubwa ili kuleta ushindi huo. Kiasi kikubwa cha pesa, nyenzo na umwagaji damu ulitumika kupata ushindi, na, ingawa ni vigumu kutoa takwimu halisi, ni sawa kukadiria kuwa zaidi ya watu milioni tatu ya waliokuwa katika Utawala wa kikoloni wa Kiingereza walihudumiwa, na kwamba inawezekana zaidi ya watu 500,000 waliangamia.¹⁰ Wakati Tawala zenye walowezi weupe za Kanada, Australia na New Zealand hutawala masimulizi ya kawaida ya Himaya nyakati za vita, ukweli ni kwamba michango yao mikubwa (ya zaidi ya wanaume na wanawake milioni 1.1) ni sehemu moja tu ya sehemu kubwa zaidi ya masimulizi ya ulimwengu.¹¹

Kwa mfano, Jeshi la India peke yake lilitoa zaidi ya wanaume milioni 1.2, na wanajeshi wake walipelekwa kwenye medani zote kuu za vita na kufanya theluthi mbili ya wafanyakazi wote wanaohudumia Mesopotamia.¹² Katika kipindi chote cha vita, karibu wanaume 1,200 walihudumia Kikosi cha West India (WIR), na zaidi ya 16,000 na Kikosi cha British West Indies (BWIR) huko Ulaya, Misri, Palestina, Afrika Mashariki na Magharibi, na Mesopotamia.¹³ Ingawa hawakuwa watu wa Himaya ya Uingereza hasa, wanaume 100,000 walitayarishwa kwa kuhudumia Uingereza katika Kikosi cha Wafanyakazi cha

⁹ Hii imehesabiwa kutokana na idadi ya sasa ya ya maadhimisho ya kumbukumbu za Uingereza zilizotajwa katika hifadhidata za CWGC za majeruhi ukiondoa takwimu za Koloni za Ufalme. Tazama maelezo 10 hapo chini.

¹⁰ Hifadhidata za majeruhi wa CWGC zina majina ya watu 1,063,137 waliotajwa kuwa walikufa katika Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia, 230,866 kati yao walihudumia vikosi vya India, Kanada, Australia, New Zealand na vikosi vya Afrika Kusini. Majeruhi ya vitengo vya Koloni za Ufalme - kama zile zilizokuzwa barani Afrika au West Indies - haziwezi kugawanywa kinchi au kieneo la asili ndani ya hifadhidata lakini zinahesabiwa chini ya jumla ya Uingereza. Ili kupata majeruhi hawa utahitaji kutafuta kitengo kwa kitengo. Takwimu zaidi ya 500,000 zilizotolewa hapa zimetokana ns jumla ya majeruhi hawa wote pamoja na makadirio ya wale ambao CWGC haina majina yao - angalia Sehemu ya 1 (ii).

¹¹ Uandikishaji wa kukadiria nchi kwa nchi: Kanada: 620,000; Australia: 380,000; New Zealand: 100 000.

¹² Kwa kampeni huko Mesopotamia, jeshi la India lilitoa wanaume 588, 717 - wanajeshi 295, 565 na 293, 152 wasio wapiganaji. Tazama *India's Contribution to the Great War* (Calcutta: Government of India, 1923), uk. 79–80, 96–7; Roy, Kaushik, *Indian Army and the First World War: 1914–1918* (Oxford: Oxford University Press, 2018), pp. 56, 342–3.

¹³ Smith, Richard, 'The multicultural First World War: Memories of the West Indian contribution in contemporary Britain', *Journal of European Studies*, Vol. 45, Na. 4 (2015), pp. 349–50.

Kichina, wakitumika zaidi Ufaransa kuanzia mwaka 1917.¹⁴ Mahali pengine, ambapo vita vilitegemea zaidi kazi, mahitaji ya nguvukazi yalikuwa hayana kikomo. Kwa Nyasaland (sasa Malawi), kwa mfano, inakadiriwa kuwa labda asilimia 83 ya nguvu kazi iliyopo - jumla ya wanaume 210,000 - walitumika kama wanajeshi au kama ilivyokuwa kawaida, kama wapagazi katika kampeni ya Afrika Mashariki.¹⁵ Kwa upana zaidi, vikosi vya Uingereza vingeweza kuajiri zaidi ya wanajeshi 50,000 wa Kiafrika na labda zaidi ya wapagazi milioni moja wa Kiafrika katika mapigano yale yale - wengi wao mwisho walitumikia pande zote mbili.¹⁶ Ingawa orodha hii si kamili, inaweza kuanza kuonyesha upana wa ajabu wa vita hivi na jamii zilizoguswa.

Ingawa ni wazi kwamba idadi kubwa ya watu waliotawaliwa na wakoloni walijitolea katika Himaya ya Uingereza, ndani ya maeneo kadhaa - lakini haswa Misri na makoloni ya Afrika Mashariki na Afrika Magharibi (pamoja na koloni za Ujerumani zilizochukuliwa na Waingereza) - pia idadi kubwa inaweza kuwa ililazimishwa au ilioandikishwa kwa nguvu na mamlaka ya jeshi na wakoloni. Hii inaweza kuhusisha vitisho vya kisiasa na kiuchumi, ubabe, wizi na, wakati mwingine, utekaji nyara wa watu wengi.¹⁷ Ndani ya Misri peke yake, imependekezwa kwamba karibu asilimia 75 ya wanaume 327,000 waliohudumia walijajiriwa kwa nguvu.¹⁸ Katika kesi hizi, inaonekana kwamba hawakujali jinsi walivyopatikana ilmradi wapatikane.

Licha ya michango hii muhimu katika jitihada za shughuli za vita za Himaya ya Uingereza, mengi huzungumzwa kwa nadra na ni nadra kwa hasara ya maisha kutenganishwa katika

¹⁴ Fawcett, Brian C., 'The Chinese Labour Corps in France 1917-1921', *Journal of the Hong Kong Branch of the Royal Asiatic Society*, Vol. 40 (2000), p. 50.

¹⁵ Wabebaji au wapagazi walikuwa wanaume walioajiriwa kusafirisha vifaa vya vita ambapo magari au wanyama hawakufaa au hawakupatikana. Hodges, G.W.T., 'African Manpower Statistics for the British Forces in East Africa, 1914-1918', *Journal of African History*, Vol. xix, Na. 1 (1978), pp. 103, 113; pia tazama *Statistics of the Military Effort of the British Empire during the Great War, 1914-1920* (London: HMSO, 1922), p. 382.

¹⁶ Hodges, 'African Manpower Statistics', p. 115.

¹⁷ Tazama Killingray, David and Matthews, James, 'Beasts of Burden: British West African Carriers in the First World War', *Canadian Journal of African Studies*, Vol. 13, No. 1/1 (1979), uk. 13-4; Page, Melvin, 'The War of *Thangata*: Nyasaland and the East African Campaign, 1914-1918', *Journal of African History*, Vol. xix, No. 1 (1978), pp. 87-100.

¹⁸ Killingray, David, 'Labour Exploitation for Military Campaigns in British Colonial Africa 1870-1945', *Journal of Contemporary History*, Vol. 24, No. 3 (1989), p. 485.

jumla ya pamoja. Kwa kweli, kutokana na muundo wa hifadhidata ya majeruhi ya CWGC, katika kesi nyingi kazi ya kutafiti haitaruhusu takwimu hizi za kitaifa za majeruhi kutenganishwa kutoka jumla ya 'Uingereza'.¹⁹ Angalau sehemu ya shida hii ya utambuzi imetokana na Falsafa za Kiulaya ambazo zimedumu na kutawala utafiti wa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia na havitoi kipaumbele kwa michango anuwai, ambayo bila shaka kama ilivyotegemewa vilifanyika mbali na Medani ya Mapambano ya Magharibi. Walakini, njia ambayo wanaume hawa wanahesabiwa kama majeruhi na kuadhimishwa - au, bila shaka, kutoadhimishwa - na CWGC kumechangia kukosekana kwa taarifa ya pamoja kuhusu mambo waliyoyafanya.

ii. Kuelezea shida

Kama uchunguzi wa awali wa maswala yanayoweza kuibuka, ripoti hii haingeweza kutoa kielelezo kamili cha jumla ya idadi ya majeruhi walioadhimishwa bila usawa au wasioadhimishwa kabisa na CWGC. Kinachofuata ni makadirio yanayotokana na utafiti wa awali.

Kwanza, ushahidi uliowasilishwa kwa Kamati hii unaonyesha kwamba, ulimwenguni, kuna kati ya majeruhi 45,000 na 54,000 waliotajwa au walioshughulikiwa tofauti na wale waliouawa huko Ulaya. Ikiwa tungechukua idadi kubwa zaidi, hii ingeweza kufikia asilimia 22 ya vikosi vyote vinavyojulikana vya kikoloni na vikosi vya Utawala ambavyo vilipewa kumbukumbu fulani iliyotambulika na IWGC. Labda cha kushangaza zaidi, takwimu hii inajulikana kujumlisha pamoja zaidi ya nusu ya Wahindi wote waliokufa na walioadhimishwa ulimwenguni.²⁰ Mifano ya maana ya jambo hili, pamoja na sababu za kisasa zilizotolewa zilizofanya watu kutafautishwa, zimeelezwa katika Sehemu ya 3 (iii)

¹⁹ Tazama maelezo 10 hapo chini. Jinsi data hii inavyowasilishwa inaonyesha njia ambayo kazi ya Tume inalipwa, ambayo ni mchango kutoka kwa serikali husika kulingana na idadi ya makaburi yaliyotunzwa. Kwa kuwa serikali ya Uingereza inashughulikia gharama za kudumisha makaburi ya wale ambao sio wa Utawala, hifadhidata inaonyesha majeruhi hawa kama sehemu ya vifo vya Uingereza. Kama ilivyotamkwa hapo awali, wanaweza kutofautishwa katika utafiti wa vikosi binafsi.

²⁰ Jumla ya maaskari katika vita vya ukoloni waliokufa wanaoadhimishwa hivi sasa na CWGC, ambao hawahusiki na ile idadi ya watu 230,866 inayohusishwa na vikosi vya India, Kanada, Australia, New Zealand na Afrika Kusini ni 12,459, hivyo kufanya jumla kuwa 243,325. Jumla ya Wahindi waliokufa waliotajwa kwenye hifadhidata ya Tume ni 73,927. Angalia Kiambatisho 1 cha idadi ya majeruhi wa India walioadhimishwa bila usawa.

ya waraka huu. Walakini, kwa vitendo, takwimu hii inahusiana na aina ya maadhimisho ya ukumbusho wa saba kwa waliopotea (tano kati ya hizo zimerekebishwa na CWGC katika miongo miwili iliyopita) na uamuzi wa makusudi wa kuacha makaburi mengine ili kuadhimisha kumbukumbu ya pamoja.²¹

Maswala yanayojulikana kuhusu kumbukumbu kwa waliopotea ni pamoja na:

- Majeruhi 38,696 wa Kihindi ambao walikuwa au bado wanaadhimishwa kwa idadi yao kwenye kumbukumbu huku majina yao yakiwa kwenye sajili za kumbukumbu tu. Hii ni pamoja na Ukumbusho wa Basra nchini Irak, kumbukumbu ya asili ya Port Tewfiki huko Misri na kumbukumbu za pamoja za Waingereza na Wahindi huko Nairobi na Dar es Salaam.²²
- Kuna jumla ya majeruhi 2,692 wa Afrika Magharibi na Wachina ambao majina yao yamewekwa kwenye sajili za kumbukumbu tu, bila kitu chochote kuandikwa kwenye makaburi yenyewe, huko Nigeria, Sierra Leone na Hong Kong.²³

Masuala yanayojulikana kuhusu kumbukumbu za makaburi ni pamoja na:

- Kuna majeruhi 3,328 wasio Wazungu katika Afrika Mashariki, Misri, na Mashariki ya Kati ambao waliadhimishwa au kujengewa kumbukumbu za makaburi, iwe kwa nambari au kwa majina, ingawa makaburi ya kibinafsi yalikuwepo ndani ya maeneo ya makaburi.

Sehemu ya mwisho ya hesabu hii inaunda makadirio ya juu na ni vigumu zaidi kupata hesabu sahihi kwani haiwezekani kujua ni wangapi kati ya wanaume hawa waliwahi kuwa na kaburi linalotambulika. Hata hivyo, wakati mwingine, IWGC ilikuwa na sera ya kutelekeza maziko mengine na kuchagua kumbukumbu za pamoja. Masuala yanayoweza kujitokeza ni pamoja na:

²¹ Tazama Jedwali A2 hadi A6 katika Kiambatisho 1 kwa orodha kamili ya takwimu zinazofuata na tarehe za masahihisho, pale inapowezekana.

²² Kati ya kumbukumbu zilizotajwa, tatu za mwisho sasa zina majina ya wafu kufuatia miradi ya awali ya CWGC. Uamuzi bado haujafanywa kuhusu Ukumbusho wa Basra, haswa kwa sababu ya kukosekana kwa utulivu huko Irak.

²³ Hizi ni takwimu za kumbukumbu pale awali zilipojengwa.

- Kiasi cha zaidi ya watu 9,061 wa Afrika Magharibi, Afrika Mashariki na Wahindi ambao maeneo yao ya kuzikwa yangeweza kujulikana lakini kufuatana na suala la sera, yalitelekezwa na waliachwa ili waweze kuyaadhimisha kwenye kumbukumbu za pamoja kwa jina, haswa katika Afrika Magharibi, Zambia, Iran na India.

Tena, kama Sehemu ya 3 (iii) inavyoelezea kwa undani zaidi, makadirio ya juu yanatumiwa kwa ufahamu kwamba mengi ya mazishi haya hayakujulikana kamwe na IWGC. Walakini, yalitokea katika maeneo ambayo shirika lilitunga sera ya kuweka kumbukumbu za pamoja kwa vikundi maalum, na hivyo halikutafuta kabisa mazishi yao na liliamua kuachilia yale ambayo tayari iliyafahamu.

Jambo hili la pili lenye utata zaidi kuliko hesabu zilizo hapo juu, ni lile linalojumuisha majeruhi ambao hawakuadhimishwa kwa kuwekewa jina au kuna uwezekano hawakuadhimishwa kabisa. Wakati tofauti zote katika shughuli za kuadhimishwa zimezingatiwa na Tume hii, na zote zimeathiri mapendekezo ambayo yametolewa, ni makundi haya ya mwisho ambayo yanaleta changamoto kubwa. Kumbukumbu zisizo na majina katika adhimisho za kijumla zilifanywa kwa sababu anuwai zilizofanyiwa utafiti katika Sehemu ya 3 (iii) katika ripoti hii, lakini kuna uwezekano athari yake ni kubwa. Pamoja na kuwakatalia majeruhi hawa mahali pa kuwaadhimisha binafsi, matokeo haya pia yameficha gharama halisi ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia kwa jamii maalum. Matokeo yake ni kwamba, jumla ya watu waliokufa vitani iliyowasilishwa na utafutaji wa majeruhi wa umma wa CWGC - ambayo imeweza kuhesabu majina yanayopatikana kwenye hifadhidata yake tu- sio sahihi. Yafuatayo ni makadirio ya idadi ya majeruhi wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia ambao hawakuadhimishwa kwa majina, taarifa inatokana na ushahidi uliowasilishwa kwa Tume hii pamoja na mahesabu yaliyofanywa mahali pengine.

Kwa wakati huu, CWGC inaadhimisha kwa majina majeruhi 1,063,137 wa Himaya ya Uingereza kutoka Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Mapungufu yaliyotambuliwa ndani ya Afrika Mashariki ni pamoja na kumbukumbu tatu zisizo na majina zilizopatikana Dar es Salaam, Mombasa na Nairobi, pamoja na Ukumbusho wa Abercorn huko Zambia,

ambao umewekwa kwa ajili ya wanajeshi wa Afrika na wapagazi ambao walikufa wakati wa mapigano kwenye medani hiyo.²⁴ Wakati wa ujenzi, IWGC iliamini hawa waliwakilisha wanajeshi 5,000 waliopotea na wapagazi kati ya 40,000 na 50,000.²⁵ Wakati utafiti uliunganishwa na ripoti hii umeweza kupata majina ya zaidi ya wanajeshi 1,400 na wasio wapiganaji kutokana na mazishi na rekodi zingine zilizopatikana ndani ya kumbukumbu za CWGC na vyanzo vingine, zaidi ya askari 4,200 wa King's African Riflemen (KAR) pekee wanajulikana kuwa walikufa katika vita na, kwa sasa, Tume haina maelezo kuhusu wengi wao.²⁶ Kama itakavyoonyeshwa katika Sehemu ya 3 (iii) ya ripoti hii, katika mfano mmoja katika miaka ya 1920 ni wazi kwamba wafanyakazi wa Tume wangeweza kupata angalau majina ya wanajeshi 5,000.

Zoezi la kuhesabu idadi kamili ya wapagazi waliopotea kwenye medani hii ni ngumu zaidi, lakini wakati huo huo ni kubwa zaidi. Kwa mfano, ripoti ya Desemba 1919 na Luteni-Kanali Oscar Watkins, kamanda wa Ofisi ya Wafanyakazi wa Kijeshi katika Afrika Mashariki, ilihesabu kuwa watu 38,642 walikuwa wamekufa kati ya jumla ya watu 485,168 waliotolewa kutoka maeneo ya British East Africa (sasa Kenya), German East Africa (sasa Tanzania, Burundi, Rwanda), Portuguese East Africa (sasa Msumbiji), Uganda na

²⁴ Mwanzoni mwa miaka ya 1920, serikali ya kikoloni nchini Uganda iliunda kumbukumbu ya kijumla huko Kampala iliyojengwa kwa ajili ya kuwakumbuka wanajeshi Wakizungu 6,000 na askari wa Uganda na wapagazi waliokufa katika mapambano nao hawakuwa na makaburi yanayojulikana. Hii ilijengwa kibinafsi na kulipiwa na michango ya umma, kwani IWGC ilijulishwa mnamo 1923 kwamba pesa ambazo walikuwa wamepanga kutoa - jumla ya £275 - hazikuhitajika. Licha ya kutolipa au kutoikubali rasmi kumbukumbu hiyo, IWGC iliitambua kuwa 'kumbukumbu sahihi ya Waliopotea kutoka makabila ya Uganda.' Tazama CWGC/1/1/9/D/33, pp. 22-55; CWGC/1/1/10/E/14.

²⁵ Takwimu zilizokusanywa na Ofisi ya Vita na kuchapishwa mnamo 1922 ziliweka idadi ya wanajeshi wa Kiafrika waliokufa kutokana na kampeni ya Afrika Mashariki kuwa 4,300 - kati yao, 1,029 waliuawa, 348 walikufa kwa majeraha na 2,923 walikufa kwa magonjwa. Walakini, jumla ya wafuasi wa Kiafrika na wasio wapiganaji walioorodheshwa kama wafu imetofautiana katika ripoti hiyo. Kwa mfano, takwimu moja ilisema 44,635 wamekufa na wengine 764 hawapatikani, nyingine iliorodhesha 48,000 kuwa ndiyo waliokufa. Tazama *Statistics of the Military Effort of the British Empire during the Great War, 1914-1920* (London: HMSO, 1922), pp. 240, 302, 382.

²⁶ Takwimu za majeruhi za KAR zilizohifadhiwa na Ofisi ya Rekodi za Vita huko Nairobi ziliuliziwa na vikosi hivyo na kuonekana kuwa ni vya chini sana. Wakati huo, walizidi 4,200 kwa safu zingine pekee. CWGC/1/1/10/E/14, 'Barua: J.N. Cormark kwa Mkurugenzi wa Rekodi', 20 Desemba 1923. Kando ya wanaume hawa 1,400 kuna karibu majina 300 ya Wahindi, Wacypriot, Wafiji na Waingereza yaliyogunduliwa na timu ya utafiti ambayo kwa sasa hayajaorodheshwa kwenye hifadhidata ya majeruhi ya Tume.

Zanzibar.²⁷ Walakini, takwimu hizi hazikuwa za mwisho na hazikujumuisha wapagazi wote waliochukuliwa kutoka katika kila eneo, na hawakujumuisha wale walioorodheshwa kama waliopotea.²⁸ Kwa hivyo, makadirio ya baadaye yaliongezeka mara dufu, na kwa mfano G.W.T. Hodges, akidokeza kwamba angalau watu 94,725 waliuawa au walikufa.²⁹ Leo, kutokana na mianya na mapungufu ambayo yanajulikana kuwamo katika rekodi ya kisasa, wanahistoria wanakubali kwamba idadi ya karibu 100,000 inawakilisha idadi ndogo ya vifo, ingawa wengine wamepata takwimu zilizokadiriwa zinazojumuisha watu walioshindwa kuendelea na mapambano (takwimu ambazo zinaweza kujumuisha aina yoyote ya ulemavu au kutoroka) na kuonyesha kwamba jumla ya idadi inaweza kufikia, au hata kuzidi vifo 300,000.³⁰ Kwa madhumuni ya hesabu hii, idadi ya pamoja ya wanajeshi wa kiafrika na wapagazi waliouawa au kufa kutokana na shughuli zilizofanywa Afrika Mashariki imekadiriwa kuwa kati ya 100,000 na 300,000.

Ukumbusho wa Giza huko Misri umeleta tatizo kama hili. Maadhimisho ya wale waliopotea kutoka Kikosi cha Wafanyakazi cha Misri na Kikosi cha Usafiri wa Ngamia, hufanywa bila ya majina yao au hata kupendekeza idadi iliyopotea. Makadirio kadhaa ya hivi karibuni yameweka takwimu hii kuwa zaidi ya 10,000, ingawa vyanzo vingine vinaonyesha kuwa idadi hii ni ndogo.³¹ Kwa kweli, kwa kuchukua wastani wa kiwango cha

²⁷ Vifo zaidi 1, 844 viliorodheshwa kwa watu 9, 768 waliopatikana nchini Sierra Leone, Nigeria na Ushelisheli. Wao wametengwa katika jumla hapo juu kwani wanaume hawa waliadhimishwa na IWGC ndani ya nchi yao ya asili. Tazama TNA, CO 533/216, 'Ripoti ya Luteni-Kanali O.F. Watkins, Mkurugenzi wa Kazi ya Kijeshi kwa B.E.A. Kikosi cha Utabiri katika kipindi cha Agosti 4, 1914 hadi Septemba 12, 1919', Kiambatisho 1, Jedwali 6.

²⁸ Wapagazi walioajiriwa na Jenerali Northey 'Norforce' walikuwa tofauti na wale walioletwa na Watkins. Katika kumbukumbu ya shajara ya vita kutoka 1 Oktoba 1917, yeye aliweka idadi yao kuwa 30,000. Imependekezwa pia (ingawa haijaonyeshwa) kwamba Watkins inawezekana Watkins alikuwa msimamizi wa wafuasi wa jeshi wawili tu kati ya kila watano katika kampeni hiyo. Tazama TNA, WO 95/5330/1, 'East Africa, HQ Norforce, Nyasaland and North-Eastern Rhodesia Frontier Force', pp. 58-9; Hodges, 'African Manpower Statistics', p. 103.

²⁹ Wakati wa mparaganyiko huu bado kulikuwa na mapungufu kutokana na ukosefu wa rekodi zilizosalia. Tazama Hodges, 'African manpower statistics', p. 116.

³⁰ Ukosefu wa nyaraka hufanya takwimu hii ya juu kutegemea sana ushahidi wa kimazingira. Ili kuelewa undani wa takwimu hizi, na vile vile viungo vya kihistoria husika, angalia Jedwali A1 katika Kiambatisho 1.

³¹ Tazama Fuchs, Ron, 'Sites of Memory in the Holy Land: The design of the British war cemeteries in Mandate Palestine', *Journal of Historical Geography*, Vol. 30 (2004), uk. 650; Starling, John and Lee, Ivor, *No Labour, No Battle: Military Labour during the First World War* (Stroud: Cambridge University Press, 2009), pp. 270-9.

vifo kwa wanaume elfu walioajiriwa kutoka Januari hadi Machi 1918, wakati janga la 'homa inayojirudia' lilipolipuka huko Palestina, inaweza kukadiriwa kuwa zaidi ya watu 10,000 walikufa wakati wa miezi hiyo mitatu tu.³² Wakati majadiliano yalipofanywa kwa mara ya kwanza na Makamishna wa IWGC mnamo Desemba 1920, ilibainika kuwa hasara katika vikosi hivi ilikuwa nzito na, ingawa idadi kamili ya waliokufa ilikuwa haijulikani, iliaininika kuwa zaidi ya watu 16,000.³³ Zaidi ya mwaka mmoja baadaye mnamo Januari 1922, wakati uamuzi wa mwisho ulipochukuliwa juu ya aina ya ukumbusho, ilibainika kuwa jumla ya wahanga waliopaswa kuadhimishwa ilikuwa 'takriban 50,000'.³⁴ Hata takwimu hii ingebadilika, na IWGC haikuwa na uhakika juu ya usahihi wake. Wakati ripoti zake za kila mwaka katika miaka ya 1920 zilizungumzia mara kwa mara juu ya majeruhi 40,000-50,000 wa Afrika Mashariki, hawakutaja tena makadirio yoyote ya Giza hadi muongo uliofuata. Ilipozungumziwa katika Ripoti ya kumi na mbili ya mwaka (1930-1), idadi hiyo ilikuwa imeshuka tena kufikia kiwango cha chini cha 10,000.³⁵ Kwa hivyo, inahitaji kutambuliwa kuwa idadi ya Wamisri wanaoadhimishwa na Ukumbusho wa Giza bado si sawa kama ilivyo idadi ya wapagazi wanaokumbukwa Afrika Mashariki. Kwa madhumuni ya hesabu hii, hata hivyo, ripoti hii inachukua takwimu za asili zilizowekwa na IWGC mnamo 1920 kuunda makadirio kati ya majeruhi 16,000 na 50,000.³⁶

³² Kiwango kinachokadiriwa cha kifo kwa kila 1,000 ndani ya Kikosi cha Wafanyakazi wa Misri, na nguvu ya jumla kwenye mabano, ilikuwa: January 1918, 53,4 (59, 135); February 1918, 96.1 (62, 921); March 1918, 111.9 (64, 672). Tazama Caddy, Peter, *British Policy and Egyptian Unrest 1914-1920* (Jarida la PhD, School of Oriental and African Studies, 1982), pp. 254-5.

³³ CWGC/2/2/1/28, Mkutano wa Tume Na.28, 20 Desembar 1920, pp. 3-5; ndani ya Ripoti ya Pili ya Mwaka ya IWGC, ilisemekana kwamba kumbukumbu ya jumla ilipangwa 'kwani hazikuhifadhiwa kumbukumbu sahihi za majeruhi' wa Kikosi cha Wafanyakazi wa Misri na Kikosi cha Usafiri wa Ngamia. Tazama *Second Annual Report of the Imperial War Graves Commission, 1920-1921* (London: HMSO, 1921), p. 8.

³⁴ Tazama CWGC/2/2/1/41, *Mkutano wa Tume Na.41*, 17 Januari 1922, pp. 8-9.

³⁵ Ndani ya Ripoti za Mwaka za IWGC 2-3, jumla ya 'Wafuasi wa Kiafrika' waliokufa Afrika Mashariki waliaininika kuwa takriban 50,000. Ndani ya Ripoti ya Mwaka ya 8-11, idadi ya awali ya watu 45,000, iliyoshushwa hadi 42,318, iliwekwa ndani ya mkusanyiko ulioorodheshwa wa Jumla ya idadi iliyoadhimishwa. Kutoka Ripoti ya Mwaka ya 12 (1930-31), idadi kubwa ya watu hao iliongezwa kwenye jumla ya kumbukumbu nchini Kenya. Kwa Misri, ongezeko kubwa moja tu lilitokea katika Ripoti ya 12 ya Mwaka, wakati ziada ya nyongeza ya watu 10,000 iliyoongezwa kwenye jumla. Kwa kuzingatia jumla ya kumbukumbu kwenye kumbukumbu zingine kote Misri, tunaweza kudhani ongezeko hili linaweza kuhusishwa na Giza - hii, hata hivyo, haikuwekwa wazi au kuelezewa. Tazama *Twelfth Annual Report of the Imperial War Graves Commission, 1930-1931* (London: HMSO, 1932), pp. 46.

³⁶ Utafiti zaidi umepangwa kuhusiana na shughuli za IWGC ndani ya Misri wakati wa awamu zilizofata za mradi huu.

Mwishowe, wakati hesabu kamili imejaa utata, kilicho na uhakika ni kwamba idadi ya waliopotea ilikuwa ya juu sana na idadi ya wanaokumbukwa binafsi ipo chini sana. Tena, kama ilivyo kwa wanajeshi waliopotea, ni muhimu kutambua kwamba ripoti ya Watkins juu ya Ofisi ya Wafanyakazi wa Kijeshi wa Afrika Mashariki inaonyesha kwamba orodha za kina za wale waliokufa chini ya amri yake zilikusanywa na kupelekwa kwa Wakuu wa Wilaya kuwajulisha jamaa na kuwarudishia vyao na malipo.³⁷ Orodha hizi hazionekani kama zilitafutwa au kama zilipatikana na IWGC.

Mwishowe, ingawa muda haujaruhusu kufanya uchunguzi kamili wa rekodi au uchunguzi wa usahihi wao, pia kuna maoni madhubuti kwamba takwimu za majeruhi zilizotolewa na Jeshi la India kufuatia Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia zilikuwa hazijakamilika. Katika hatua hii ni mapema mno kutabiri kwa usahihi ni wanaume wangapi hawakuweza kuadhimishwa, lakini inaweza kufikia mamia ya maelfu.

Kama ilivyoielezwa hapo awali, wakati wa ujenzi wao, IWGC waliamini kwamba hizi kumbukumbu zisizo na majina zilizojengwa Afrika ya Mashariki na Misri zilijumuisha kati ya majeruhi 66,000 na 100,000. Leo, kwa kutumia makadirio yaliyoainishwa hapa na katika Jedwali A1 katika Kiambatisho 1, inakadiriwa kuwa takwimu hasa ni wapiganaji na wasio wapiganaji wa Himaya ya Uingereza 116,000. Wakati labda haiwezekani kuthibitisha kwa njia yoyote ile kwa sababu ya ukosefu wa maandishi katika makaratasi, kwa kuchukua makadirio ya juu, kwa sasa haiwezi kutoaminika kwamba takwimu hii inaweza kuwa kubwa kiasi cha 350,000. Takwimu hizi, kama njia ya ulinganisho, zingefikia kati ya asilimia 11 na 33 ya wale ambao kwa sasa wameorodheshwa katika hifadhidata ya majeruhi ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia.

³⁷ TNA, CO 533/216, 'Ripoti ya Luteni-Kanali O.F. Watkins, Mkurugenzi wa Kazi ya Kijeshi kwa B.E.A. Kikosi cha Utabiri katika kipindi cha Agosti 4, 1914 hadi Septemba 12, 1919', pp. 18-19.

SEHEMU 2 - MAJUKUMU NA WAJIBU WA IWGC

i. Uanzishwaji, kanuni na umuhimu wa Medani ya Mapambano ya Magharibi

Sababu ya msingi ya kuanzishwa kwa IWGC ilikuwa gharama kubwa ya kibinadamu ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Kamwe ulimwengu haukuwahi kushuhudia mzozo uliofikia umwagaji damu kama huo, na kamwe hawakuwahi kuita idadi hiyo ya watu kutoka katika Himaya ya Uingereza ili kupigania ushindi. Vita vya kipekee vilizaa mahitaji ya kipekee ya kutambua jinsi watu walivyojitoa mhanga, na hii ilikuwa kwa sababu ya hali hizi za kipekee kwamba hakuna kitu kilichopendekezwa na IWGC mnamo 1917 kilichokuwa cha kawaida. Ingawa haikuwa jambo geni kwa kwa vikosi vya Uingereza kuadhimisha ushindi au kuabudu viongozi, kihistoria askari aliyekufa hakupokea utambuzi wa kudumu uliokuwa wa kibinafsi kutoka kwa serikali kwa njia ya mazishi au kumbukumbu. Matokeo yake ni kwamba, wazo lenyewe la kazi ya Tume lilikuwa jambo jipya.

Ijapokuwa kama ilivyotajwa, kujitolea kwa kuadhimisha kwa kila majeruhi wa vita kwa jina kulipokelewa vizuri, maamuzi mengine kadhaa hayakuwa bila ubishi. Kwanza katika mabishano hayo ilikuwa njia ambayo serikali ilionekana kuchukua umiliki wa wafu. Uamuzi wa kutowarudisha waliouawa bali kuwaadhimisha walipokufa ulikuwa na athari kadhaa za kudumu na kubwa, muhimu zaidi ilikuwa mabadiliko ya viwanja vya vita vya zamani kuwa makaburi na kumbukumbu zinazofaa wafu wa Himaya. Hata hivyo, kusudi lililoendeleza uamuzi huu lilikuwa kutafuta usawa na kuwa sare katika njia ambayo majeruhi walikumbukwa - Bila ya kujali kiwango chao katika maisha ya kijamii au ya kijeshi, bila ya kujali dini yao. Kwa hoja hii ya mwisho, ni wazi kutokana na taarifa zilizotolewa katika Ripoti ya Kenya kwamba IWGC ilikubali kujitolea kwa kuwaadhimisha watu wote wa himaya kwa namna moja na kwa mujibu wa imani zao, na Tume ilishirikisha maoni na malengo haya katika chapisho linaloelezea kazi yake.³⁸ Walakini, kama

³⁸ Ingawa chapisho la Kipling lina rejea za moja kwa moja kwa 'Makaburi ya Vikosi vya Wahindi', lengo lake - kama ilivyo kwa kiasi kingine - ni kwa wale waliouawa upande wa Magharibi katika mapigano. Sehemu kubwa ya Ripoti ya Kenya ina upendeleo kama huo lakini inajumuisha nyongeza ya miezi kumi baadaye ikielezea kuongezwa kwa mpango huo katika medani zingine za vita. Ingawa hii ni pamoja na marejeleo ya Misri, Palestina, Makedonia, Gallipoli na Mesopotamia, medani za vita kwa Waafrika bado hazipo. Kipling, Rudyard, *The Graves of the Fallen* (London: HMSO, 1919); Kenyon, Lt-Kol. Bwana Frederic, *War Graves*, pp. 22-4.

itakavyoonyeshwa, kuna mifano ambapo tafsiri ya imani ya IWGC na mambo mengine yalisababisha vikundi kadhaa kufanyiwa mambo tofauti na bila usawa kwa makusudi.

Licha ya hali ya kivita ya ulimwengu na kujitolea kwa IWGC ulimwenguni, ni wazi Tume bado ilivipa kipaumbele viwanja vya vita vya mapigano ya Magharibi. Hii sehemu kuu na kitovu cha vita vya Himaya ya Uingereza ilikuwa na hesabu kubwa zaidi ya majeruhi, ukaribu wake na Uingereza na ushirikiano wa mamlaka ya Ufaransa na Ubelgiji vilihimiza kazi ya IWGC. Uwepo wake karibu zaidi na jiji kuu la kifalme, na eneo lililounganishwa kwa urahisi zaidi na ulimwengu wote kupitia mitandao ya usafiri iliyojengwa muda mrefu, ilitarajiwa kabisa kwamba watu watatembelea makaburi na kumbukumbu za maeneo ya mapigano ya upande wa Magharibi kwa idadi kubwa zaidi kuliko sehemu nyingine yoyote katika medani za zamani za vita. Wakati hii ilichukua dhana ya wageni kuwa wazungu zaidi ya wengine wote, pia kulikuwa na utambuzi wa ukweli kwamba watu wa Himaya walisafiri kwenda Ulaya kupigana vita vya Uingereza na wangeweza kufanya hivyo tena kwa ajili ya maadhimisho.

Kwa upeo wa shirika, kwa hivyo, siku zote waliamini kwamba kazi yake ingehukumiwa kutokana na eneo la mapigano la Magharibi. Medani hii kuu ilikula rasilimali za ulimwengu wakati wa vita na kupafanya kuwa lengo kuu la IWGC baada ya vita. Huku macho ya ulimwengu yakiendelea kuwalengea, ni hapo ndipo Tume ilijenga kazi zake kubwa na za usanifu, ikionyesha umuhimu wa vita huko Ulaya na gharama yake isiyo na kifani. Hili lilikuwa jambo ambalo Katibu Mkuu Msaidizi, Bwana Arthur Browne, alielezea zaidi ya mara moja, na hivyo kumaanisha kuwa sehemu nyingine, kazi ya IWGC nje ya Ulaya haikuanza hadi mwanzoni mwa miaka ya 1920.³⁹

Ucheleweshaji wa ujenzi wa makaburi na ukumbusho sehemu za mbali zaidi uliwasilisha shida mpya zilizotokana na umbali, mawasiliano, hali ya mitaa na kutokuwa na utulivu kulikokuwa kukiendelea. Baada ya vita, Mesopotamia (sasa Iraq), kwa mfano, kwa muda mfupi ilikuwa ni koloni la kilazima la Uingereza kutokama na sheria ya Ligi ya Mataifa lakini ilikuwa imerudi kwa ufalme chini ya utawala wa Uingereza kufuatia ghasia na

³⁹ CWGC/1/1/7/E/63. 'Barua: Bwana Arthur Browne kwa Waziri, Tawi la Maulizo', 3 Aprili 1923.

machafuko yaliyoendelea. Barani Afrika, kwa upande mwingine, usambazaji wa mapigano, mazishi ya mbali na changamoto za hali ya hewa zilileta shida za kipekee ikilinganishwa na maeneo ya mapigano ya Magharibi. Ingawa kijuu juu mambo haya hayakuwa dhahiri, lakini wakati mwingine shida hizi zilichangia katika maamuzi ambayo yalisababisha utofauti kutoka kwenye kanuni za msingi ambazo zilielekeza shughuli za IWGC katika maeneo ya karibu na nyumbani.

Hadi hivi karibuni, masomo ya kina zaidi ya IWGC na kazi yake yamezingatia juhudi na mafanikio yake huko Ulaya. Hapa, chini ya shinikizo kubwa na uchunguzi wa kina, ni wazi shirika lilifanya bidii kufikia malengo yaliyotangazwa hadharani. Pale ambapo hali ilikuwa ngumu zaidi na rekodi zilikuwa chache, au ambapo rasilimali na wafanyakazi walitumikishwa sana, inaonekana kwamba sheria na kanuni ambazo zilikuwa takatifu huko Ulaya ziliweza kubadilika au hata kutolewa.

ii. Mirathi ya mazishi wakati wa vita, usajili wa makaburi na ubaguzi katika maandishi ya makaratasi

Licha ya jukumu la IWGC kama shirika linalohusika na ukumbusho wa baada ya vita ndani ya Himaya ya Uingereza, kabla ya Septemba 1921 haikuwajibika kutafuta, kuweka alama na kuzingatia mazishi kwenye uwanja wa vita. Vikosi vya Uingereza vilikwenda vitani bila michakato rasmi ya kuagiza na kurekodi makaburi, jambo ambalo haraka likawa shida wakati idadi ya majeruhi ilipozidi matarajio. Zaidi ya hapo, hakukuwa na shirika rasmi la kusimamia mazishi au utafutaji wa wanaume na wanawake waliopotea. Hii ilimaanisha kwamba wengi wangezikwa na wenzao karibu na mahali walipokufa bila eneo hilo kurekodiwa rasmi, wakati wengine wangeweza kuzikwa na adui na kupata matokeo kama hayo. Huko Ulaya, hii ilisababisha makaburi yaliyotengwa na makaburi ya muda na alama za muda, ambazo nyingi zilifutwa kutokana na mapigano ya mara kwa mara kwenye uwanja mmoja. Mahali pengine, mambo bado yalikuwa na shida zaidi. Kwa Afrika Mashariki, kwa mfano, makaburi mengi - lakini haswa yale ya Wahindi na Waafrika - hayakuwekewa alama kabisa na maafisa wa jeshi la kikosi chochote cha kupigana, hivyo hapakuwa na uwezekano wa ufuatiliaji wowote kwa mamia na maelfu ya wanaume.

Kwa wale waliouawa na hawakupatikana, usumbufu ulioendelea katika uwanja wa vita ulifanya wapate uwezekano mdogo wa kupatikana kwani ardhi iliyochomwa ilimeza miili yao. Ingawa ufanisi wa usajili wa makaburi uliboreshwa jinsi vita vilivyoendelea, hali ya mapigano ilimaanisha kuwa majeruhi wengi hawangeweza kupatikana kabla ya kumalizika kwa vita. Wakati huo ulipofika, kupita kwa wakati na kutokana na sababu na utaratibu wa kifo kulimaanisha kwamba wengi hawakutambulika.

Ikiwa na asili katika kitengo cha wagonjwa wa Msalaba Mwekundu cha Uingereza, shirika la kijeshi lililojitolea kushughulika na wafu lilipokea idhini rasmi mnamo 1915. Fabian Ware ndiye mwanzilishi - mtu mbaye hapo baadaye alihusika na kuanzishwa kwa IWGC - ambayo hatimaye ingejulikana kama Kurugenzi ya Usajili wa Makaburi na Maulizo (DGRE) ilikuwa na jukumu la kutafuta, kusajili na kuzingatia mazishi katika makaburi yaliyopangiliwa na kutoa alama za kudumu. Ingetakiwa kuwa Vitengo vya Usajili wa Kaburi (GRUs) vya shirika hili viendeele kufanya utafiti katika uwanja wa vita kwa wafu na waliopotea baada ya vita. Umuhimu wa mpango huu na mpangilio ni muhimu. Kufikia Juni 1919, Fabian Ware aliripoti kuwa wafanyakazi 15,000 walikuwa wameajiriwa na DGRE kwa ajili ya kutafuta na kuzingatia makaburi huko Ufaransa na Ubelgiji, na mwanzoni mwa 1920, wanaume 9,000 walikuwa bado wakifanya kazi katika kampuni hizi za kufukua maiti. Mwisho wa kazi yao mwaka uliofuata, walikuwa wamekusanya mabaki ya zaidi ya majeruhi 200,000.⁴⁰ Timu hizi zilihusika na usajili mwingi, urejeshwaji na uzikaji ambao ulifanyika kwenye medani. DGRE iliweza kufika mbali zaidi ya eneo la mapigano la Magharibi la zamani, lakini hakuna mahali ambapo nguvu kazi hii ilikuwa sawa.

Wakati viwanja vya vita vilivyokuwa havina nafasi na vyenye ulingo kama Gallipoli vilileta matatizo yaliyotokana na wiani ya miili, huko Mesopotamia na Afrika Mashariki - ambapo mapigano yalikuwa ya kutembea zaidi na kuchukua umbali mkubwa na maeneo ya mbali - mazishi ambayo yalikuwa yanajulikana kuwapo hayakusajiliwa kwa miaka. GRU inayohusika na medani ya vita ilikuwa na maafisa 6 tu na wafanyakazi 130 walioshughulikia zaidi ya maili mraba 650,000 ya nchi saba tofauti.⁴¹ Kwa upande wa

⁴⁰ CWGC/2/2/1/13, *Mkutano wa Tume Na.13*, 17 June 1919; CWGC/1/1/7/B/47. 'Kumbukumbu: Brig-Gen E. Gibb', 19 Januari 1920.

⁴¹ *Statistics of the Military Effort of the British Empire during the Great War*, p. 344

rasilimali zilizopelekwa, tofauti na eneo ya mapigano ya Ulaya Magharibi ilikuwa kubwa, na sasa tunapoitazama historia, haishangazi kwamba matokeo ya kazi yake yalikuwa tofauti kabisa. Wakati shida zilizokabiliwa kwenye viwanja vya vita vya zamani kule Ulaya zilitokana na idadi kubwa ya majeruhi na hali ya kifo, medani za mbali zaidi zilileta changamoto za kipekee wakati wa kutafuta na kutambua wafu. Hali ya hewa na ardhi ya eneo isiyofaa ilifanya mazishi mengine yasiwezekana kufikia, wakati uharibifu wa alama za mbaao na mchwa au wizi wa mabamba ya chuma yaliweza kuwaibia wafu kitambulisho chao. Jua pia liliweza kubabua na kutoa herufi kutoka kwenye ubao wa majina, na wanyama pori na hali ya hewa viliweza kuharibu ushahidi wa mahali pa mwisho pa kupumzika maiti. Zaidi ya yote, hata hivyo, ilikuwa ubora wa kuashiria kaburi wakati wa vita na muda uliotolewa ndivyo vilivyoleta changamoto kubwa zaidi. Kucheleweshwa kwa kazi ya usajili wa makaburi ya DGRE na shughuli za IWGC baada ya vita kulikuwa na athari kubwa kwa majeruhi wa Kihindi na Kiafrika waliouawa nje ya Ulaya. Wengi wa wanaume hawa, hata hivyo, wangepotea kwa sababu mazishi yao hayakuwekewa alama zipasavyo tangu awali.

Ingawa tofauti katika mila za mazishi na usajili wa kaburi zinaweza kumaanisha mahali pa mwisho pa kupumzika kwa majeruhi hazingewekwa alama, kutofaulu kwa utawala kunamaanisha majeruhi wengine wengi hawajawahi kuripotiwa au kurekodiwa kabisa. Wakati IWGC ilipochukua umiliki wa kuandikisha kwenye makaratasi na makaburi ya DGRE ili kuanza kazi yake, kwa vyovyote vile haingewezekana kuhesabu waliokufa wote. Kwa sababu zilizoainishwa tayari, kulikuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi ambao walipotea - hii ikimaanisha wale ambao hawana kaburi lililotambuliwa - lakini hata kutoa idadi ya watu hawa ilikuwa vigumu. Kwa habari hii IWGC ilitegemea matawi ya huduma na ofisi za serikali za kikoloni, Utawala na serikali ya Uingereza, ambazo pia zilitegemea utunzaji wa kumbukumbu za wakati wa vita. Wakati mchakato huu unaonekana kufanikiwa kwa majeruhi wa Uingereza na Utawala, takwimu nyingi na orodha za majeruhi zilizotolewa na Jeshi la India na mamlaka zingine zinaonekana kuwa na kasoro. Inaonekana kwamba orodha zingine za kisasa na vyanzo vya habari kuhusu majeruhi wa ukoloni ambao waliaminika kuwepo, haikukabidhiwa kwa IWGC au kutafutwa kikamilifu na shirika.

Waandishi na wanahistoria mara nyingi walisema kwamba takwimu ambayo IWGC imeifanyia kazi ya wale wanaofikiriwa kuwa wamepotea mwishoni mwa vita ilikuwa takriban 300,000, lakini - ikiwa kama mfano wa falsafa za Ulaya - takwimu hii inaonekana kuwa imeambatanishwa sana na Eneo la Magharibi la Mapigano.⁴² Katika ripoti zilizochapishwa za kila mwaka, idadi ya waliopotea kweli iliendelea kuongezeka katika miaka ya 1920 kila habari mpya zilipopatikana, na kufikia 1934 IWGC ilionekana kukubali kuwa takwimu hizi haziwezi kuzingatiwa kuwa za mwisho - kwa sehemu kubwa kwa sababu wafu waliendelea kupatikana, na wakati mwingine kutambuliwa. Walakini, mwaka huo jumla ya 'Idadi ya wafu walioadhimishwa ambao Makaburi yao hayajulikana' ilifikia karibu 518,000, ambayo karibu 27,000 walikuwa huko Gallipoli, zaidi ya 56,000 walikuwa India na Irak, na karibu 67,000 walikuwa wameenea katika bara la Afrika (ingawa 58,493 kati ya hawa walisemekana kuwa Misri na Kenya pekee).⁴³

Kuzingatia takwimu hii ya 300,000, sio tu kwamba kumesaidia kuendeleza umuhimu ulioonyeshwa wa maeneo ya mapigano huko Ufaransa na Ubelgiji, bali matumizi ya lugha yanaficha mabadiliko kutoka kwenye ripoti za awali, ambazo zilikuwa na nafasi kwa 'makaburi yaliyotambuliwa na kusajiliwa' na 'Waliopotea', Ilijumuisha safu ya 'jumla ya majina yaliyosajiliwa'.⁴⁴ Kurahisisha muundo wa majedwali hayo yaonyeshe idadi ya waliokufa katika makaburi yaliyotambuliwa na idadi ya wafu ambao makaburi yao hayakujulikana, kuliepuka suala la wale ambao *majina* yao yaliendelea kutojulikana. Ikiwa kumbukumbu zisizo na majina zimekamiliwa katika Afrika Mashariki, Misri na Irak tangu zamani, basi inadhaniwa IWGC ilikubali kwamba katika kesi nyingi majina haya hayatajulikana kamwe. Ambapo habari kamili haijatolewa kwa Tume, ni wazi pia kwamba

⁴² Tazama, kwa mfano, Longworth, Philip, *The Unending Vigil – The History of the Commonwealth War Graves Commission* (Barnsley: Pen & Sword, 2010), pp. 84. Ni jambo la kufurahisha kutambua kwamba ujazo wa maandishi ya Longworth, uliochapishwa mwanzoni mnamo 1967, hautoi habari yoyote iliyoangaziwa katika ripoti hii. Hiyo inazungumzia kazi za baada ya vita barani Afrika kwa ukurasa mmoja na zaidi kidogo. Imekuwa na jukumu kuu katika kuendeleza toleo safi la historia ya awali ya shirika.

⁴³ *Fifteenth Annual Report of the Imperial War Graves Commission, 1933–1934* (London: HMSO, 1935), pp. 42–5.

⁴⁴ *Ripoti ya Saba ya Mwaka ya Tume ya Vita vya Himaya, 1925–1926* (London: HMSO, 1927), pp. 48–51.

sera zilizotungwa na shirika ziliruhusu majina kuachwa au kutolewa kwenye sajili badala ya kuchongwa kwenye jiwe. Kama ilivyoadiliwa tayari, maamuzi haya yamezuia utengenezaji wa idadi kamili na ya mwisho kwa wafu wanaojulikana katika Himaya ya Uingereza kwa vita hivi.

Ingawa kila wakati kulikuwa na maelezo yaliyo wazi juu ya malipo ya mashirika yanayohusika na utunzaji na kuadhimishwa kwa wafu, hata hivyo uchunguzi mdogo tu unaonyesha kuwa katika kesi nyingi, uongozi na kazi zilikuwa za zaidi ya moja, au zilihama kutoka moja hadi nyingine. Fabian Ware - nguvu iliyosababisha uundwaji wa DGRE na IWGC - labda hii ni kesi iliyo wazi zaidi, lakini pale unaposonga mbele ndivyo tofauti zilivyopotea. Tena, Afrika Mashariki inatoa mfano wa kupendeza, ambapo mkuu wa GRU alihamia IWGC kuanzisha Tawi lake la Afrika Mashariki. Ingawa hii inaweza kuonekana kuwa jambo la busara kutokana na uelewa wa George Evans wa medani na jukumu lake katika kuweka ishara kwenye makaburi kabla ya uteuzi wake, pia ilihakikisha kwamba upendeleo wake wa kibinafsi ulihamishwa pamoja naye.

SEHEMU YA 3 - MAKOSA, UANGALIZI NA DHULUMA

i. Mmemenyuko badala ya hatua

Ingawa CWGC ni shirika kubwa ulimwenguni linalohudumia zaidi ya maeneo 23,000 katika nchi na wilaya zaidi ya 150, ni makaburi na kumbukumbu za CWGC huko Ulaya ambayo hupatikana kirahisi na hutembelewa zaidi. Hizi huonyesha viwango, kanuni na maadili ambayo umma umekuja kushirikisha na CWGC- kwa sehemu kama matokeo ya njia ambayo Tume imezungumzia kazi zake, lakini pia kama kielelezo cha umuhimu wa medani wakati na baada ya vita vyote vya dunia. Maeneo haya yalipokea rasilimali nyingi za Tume na kuhudumiwa baada ya mizozo hiyo na ni kwa kazi hii ambapo Tume imekuwa ikihukumiwa katika historia. Walakini, hali ya vita viwili ambavyo Tume ilianzishwa ili kuadhimisha inamaanisha kuwa jukumu lake daima lilikuwa la ulimwengu.

Katika miongo michache iliyopita hakukuwa na uhaba wa hafla na mipango inayoangazia uwepo wa CWGC ulimwenguni na, muhimu zaidi, inayozingatia tofauti kati ya wale walio katika utunzaji wake. Makaburi na kumbukumbu kote ulimwenguni yanaendelea kudumishwa kwa viwango vya juu kabisa, na miaka mia moja ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia na maadhimisho ya miaka sabini na tano ya VE-Day na VJ-Day imeonyesha uwezo wa shirika kushirikisha umma katika historia yake na kusudi lake. Walakini, kama matokeo ya ripoti hii yanavyoonyesha, matukio haya na miradi imeonyesha ni kiasi gani cha historia ya mapema ya Tume imetakaswa au kufikirika upya katika karne ya uwepo wake. Kuliko kufanywa kitendo chochote kwa kusudi fulani, hii inaweza kuelezewa kwa mabadiliko ya mwelekeo kwa muda. Katika miaka iliyofuata vita viwili vya dunia, IWGC ilipitia vipindi vilivyotambulika kwa kazi kali ya kiutawala na kiufundi wakati ikikusanya majina ya waliokufa na kujenga makaburi na kumbukumbu. Kutokana na nguvu hii ya utekelezaji, IWGC ilibadilika na kuwa shirika la kazi ambalo kusudi lake la msingi lilikuwa, kwa kufuatilia kanuni zake, ni kudumisha maeneo haya milele. Bila uwezo au mahitaji dhahiri ya kuchunguza historia yake wenyewe, na kwa kuwa pale awali nyaraka zake zilipangwa kwa ajili ya kazi za kiutawala na si masomo, haishangazi kwamba matatizo mengine magumu zaidi yaliyohusika na uwepo wake awali yalipotea kutoka kwenye kumbukumbu za taasisi.

Muda umeweza kuonyesha mabadiliko haya tena, na uteuzi wa hivi karibuni wa wahifadhi nyaraka na wanahistoria wanaoajiriwa kikamili umeanza kubadilisha mtazamo wa shirika na pia upatikanaji wa nyaraka zinazoelezea hadithi yake. Taasisi hiyo pia haijaka bure pale ambapo maswala yamejitokeza. Kumbukumbu ya Port Tewfik huko Misri (sasa iko Heliopolis) ilijengwa tena na kufunguliwa mnamo 1980 baada ya ile ya asili kuharibiwa wakati wa Vita vya Israeli na Misri vya 1967-1973. Tofauti na ile ya asili, hata hivyo, ni kuwa hii ya sasa inayo rekodi ya majina ya wanaume 4,000 inaowaadhimisha - wote kutoka Jeshi la India, waliopotea bila makaburi yaliyojulikana huko Misri na Palestina katika Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Kama jedwali A2, A3 na A5 ndani ya Kiambatanisho 1 kilichoainishwa, mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000 majina ya Wahindi pia yaliongezwa kwenye Ukumbusho wa Waingereza na Wahindi wa Nairobi na Ukumbusho wa Waingereza na Wahindi wa Dar es Salaam (wote 2004), na pia idadi ya kuta zenye skrini kwenye maeneo ya Mashariki ya Kati, pamoja na Makaburi ya Beirut Maronite (1997), Makaburi ya Vita ya Tul Karm (1999) na Makaburi ya Waislamu ya Manara ya India (2002). Kabla ya hii, maeneo haya yote yalikuwa yameandika *nambari* tu ya Wahindi waliokufa. Vivyo hivyo, huko Nigeria, wakati serikali ilipohamisha mji mkuu wake kutoka Lagos kwenda Abuja na kujenga Makaburi mapya ya Kitaifa ya Jeshi, CWGC ilijenga tena kumbukumbu mbili ili kuunda Ukumbusho wa Abuja. Iliyojitolea kwa Wanigeria waliokufa katika vita vyote viwili vya dunia, sasa inajumuisha majina ya Kikosi cha Usafirishaji cha Nigeria, kilichoondolewa kwenye kumbukumbu ya awali na serikali ya kikoloni kwa idhini ya IWGC. Ijapokuwa masuala yanayoendelea ya usalama nchini Irak yamechelewesha maamuzi yoyote kuhusu hatua zifuatazo, katika miaka ya hivi karibuni CWGC imesahihisha na kuthibitisha majina ya Wahindi yaliyomo kwenye sajili za Kumbukumbu ya Basra, ambayo yaliondolewa kwenye mnara wakati wa ujenzi wake. Kwa kiwango kidogo, CWGC pia inaendelea kujishughulisha na miradi ambayo inatafuta wale ambao kwa sasa hawajasajiliwa lakini wanapaswa kukumbukwa, kwa mfano mradi wa *In From the Cold project*.⁴⁵

Walakini, licha ya kubaini shida na kuzirekebisha kimya kimya, ni sawa kusema kwamba, kihistoria, CWGC haikuzisaka. Vivyo hivyo, wala haijashirikisha hadharani au kurekodi

⁴⁵ <http://infromthecold.org/>.

kasoro nyingi ilizorekebisha au kukubali ukweli kwamba makosa haya yalipinga kanuni zake na mazungumzo ya usawa katika kifo. Pamoja na kuwa wanaoitika pale tukio linapotendeka kuliko kuwa watendaji, Tume pia imechukua muda kujishughulisha na matokeo ya utafiti wa nje ambao umeonyesha matatizo mengi zaidi.⁴⁶

ii. Mipaka ya usawa

Usawa katika kifo ulikuwa jiwe la msingi la sera ya IWGC na ilikuwa sababu ya msingi ya upinzani wa shirika katika shughuli ya kurudisha nyumbani. Ni katika kuangaliwa na shirika lililojitolea ndipo kujitoa kafara kwa wafu kunaweza kufanywa kuwa jambo la kawaida na kushughulikiwa katika kifo kwa usawa. Kanuni hii imekuwa ikichunguzwa sana kinadharia na kivitendo kwa mtazamo wa kijamii, haswa kuhusu idadi ndogo ya jamaa wa karibu ambao walidai kwamba wanapaswa kuwa na uhuru wa kuchukua maiti zao nyumbani. Kazi kidogo imeangalia mapungufu ya usawa katika kifo kuhusu medani za vita au yale yanayotokana na rangi ya mtu au dini, lakini hii ni matokeo ya kufanikiwa kwa sera huko Ulaya. Hii haimaanishi kuwa ni hapo tu ambapo IWGC iligundua lengo hili au ambapo ilifanya kazi kuifanya iwe kweli, lakini kwamba hali ya mapigano na rasilimali zilizotolewa hapo zilihakikisha kuwa imefanikiwa. Pale ambapo hali na habari hazikuwa nzuri, au ambapo IWGC ilihitaji kufanya kazi pamoja na mashirika mengine au mamlaka, wakati mwingine maamuzi ya makusudi yalifanywa ambayo yaliruhusu kanuni za kuwa sare na kuleta usawa zitupiliwe mbali hivyo kupuuzwa kwa wanaoadhimishwa.

Wakati vita vilipokuwa vikipiganwa, IWGC ilikuwa imesambaza habari juu ya jukumu lake na madhumuni kwa zile medani sehemu ambazo hawakuwapo wao. Mnamo Juni 1918 nakala ya ripoti ya Kenyon iliyotajwa hapo awali ilitumwa kwa Amiri Jeshi Mkuu wa Afrika Mashariki, Luteni-Jenerali wa Afrika Kusini Bwana Jacob Louis van Deventer. Akijibu ripoti hiyo mnamo Oktoba 26, 1918, chini ya kichwa cha habari 'Kushughulikiwa kwa Usawa', alirejelea idadi kubwa ya Wahindi na Waafrika ambao walizikwa katika maeneo ya uwanja wa vita lakini makaburi yao hayakutambulika. Labda hii ilikuwa mara ya kwanza kutajwa kwa suala hili huko barani, suala ambalo kwa kweli lilihusu idadi kubwa ya maziko ya Waafrika na Wahindi kutoka vitani. Kilichofuata, hata hivyo, kikaja kuwa na athari kubwa

⁴⁶ Kwa muhtasari wa kazi hii, angalia tanbihi 6.

juu ya njia ambayo wengi wa wanaume hawa wangepadhimishwa. Van Deventer alisema kuwa wengi wa Waafrika wanaohusika walikuwa wameajiriwa kutoka katika vikundi vya kikabila ambavyo vilikuwa na 'kanuni za kishenzi na hawakuzika wafu wao, mila zao zilikuwa ni kuweka maiti porini ili waliwe na fisi'.⁴⁷ Baadaye kidogo, mnamo Januari 1920, George Evans - afisa anayeamuru Kitengo cha Usajili wa Makaburi katika Afrika Mashariki na baada ya muda akawa Naibu Mkurugenzi wa Ujenzi wa IWGC huko huko - alielezea kwamba karibu asilimia 95 ya mazishi ya Ulaya yalikuwa yamepatikana na kupewa vyuma vya misalaba vya muda mfupi. Shughuli kama hiyo, alisema, haikuwezekana kwa Wahindi na Waafrika, haswa kwa sababu hawakuwa wamewekewa alama ya kutosha wakati wa vita. Kiwango cha upotezaji pia kiligusiwa, na makadirio ya Waafrika 50,000 wa vitengo vya wafanyakazi wakiwa wamekufa kutokana na magonjwa na sababu zingine. Kama vile van Deventer alivyosema, yeye pia alirudia imani kwamba Waafrika wengi 'hawana aina yoyote ya hisia katika kuashiria makaburi ya wafu wao, na, kwa sababu hiyo, alisisitiza kuwa ujenzi wa kumbukumbu kuu utakuwa njia bora zaidi na ya kiuchumi ya kuadhimisha.⁴⁸ Hukumu za kijuujuu kama hizi, ambazo zilichagua kupuuza tofauti na wingi wa imani, utamaduni na mila huko Afrika nje ya mila za Kikristo na Kiislamu, zilichukua jukumu muhimu katika kuunda sera za IWGC ambazo zilisababisha watu kutofautishwa.⁴⁹

Akimwandikia Mkurugenzi wa Kumbukumbu wa IWGC mnamo 1925, Lord Arthur Browne - Katibu Mkuu Msaidizi wa shirika hilo - alisema kuwa, 'wamekuwa na maoni kama ya Makamu Mwenyekiti kwamba usawa unapaswa kutolewa kwa wanajeshi wa Uingereza na wenyeji pale tu hali inaporuhusu'.⁵⁰ Haionekani kuwa kulikuwa na sheria nzito kuhusu wakati ambapo hali ingeruhusu tofauti, lakini ni wazi kuwa kabla ya vita kumalizika, IWGC

⁴⁷ Barua ilisainiwa kwa niaba ya Van Deventer na mtumishi wake mmoja. CWGC/1/1/7/E/52, 'Barua: GOC-in-C, Vikosi vya Usafiri vya Afrika Mashariki kwa Katibu wa IWGC', 26 October 1918, pp. 14-16; <https://www.cwgc.org/media/qvylruql/the-kenyon-report.pdf>, pp. 7.

⁴⁸ CWGC/1/1/7/E/52, 'Meja George Evans, OC GRU Afrika ya Mashariki, kwa Mkurugenzi wa Kazi wa IWGC', 31 Januari 1920, pp. 73-4.

⁴⁹ Maoni kama hayo, na mpango wa kujenga kumbukumbu za jumla Afrika ya Mashariki, vilichunguzwa na kuhakikishwa na Ofisi ya Ukoloni. Tazama CWGC/1/1/7/E/52, pp. 97-8, 103-4, 118-19.

⁵⁰ CWGC/1/1/7/E/67, 'Usajili wa Kumbukumbu za Makaburi kwa Wenyeji', 24 Novemba 1925, pp. 130.

ilijua kuwa usawa kamili barani Afrika na sehemu za Mashariki ya Kati haungeweze kana kwa Waafrika na Wahindi wengi waliofariki vitani.

Kutambua majina ya waliopotea na rekodi za kutosha kutoka kwa vikosi vya jeshi na tawala za kikoloni mara nyingi ilikuwa vigumu. Waraka wa Ofisi ya Wakoloni kutoka 1925, kwa mfano, ulibaini kuwa kikosi cha Afrika Mashariki kilibadilishwa kwa kiasi kikubwa kutoka kwa rasilimali za eneo hilo, ikimaanisha kwamba mfumo wa kuridhisha wa utunzaji wa kumbukumbu haukuwepo.⁵¹ Hii haimaanishi kuwa hakuna rekodi zilizoundwa au, hakika, kwamba bado hazipo, lakini kwamba Ofisi ya Wakoloni haingeweza au haingeenda kuzitafuta.⁵² Katika hali kama hizi inaonekana kuwa Tume haikufanya hivyo pia. Mwishowe, wakati kazi bila shaka ilikuwa ngumu, ni wazi pia kuwa rasilimali chache zilipatikana kwa medani hizi za mbali na, sehemu kubwa ya kile kilichopatikana, ilitumika katika kutafuta mazishi ya Wazungu. Kama mifano itakavyoonyesha, kulikuwa na hafla katika miaka ya 1920 wakati IWGC ingeweza kupata majina au maeneo ya mazishi ya askari wa Kiafrika, lakini badala yake iliacha moja au yote mawili ili kufuatilia sera ya maadhimisho ya pamoja. Kwa upande mwingine, kwa miongo kadhaa IWGC ilifuata mamlaka ya Ufaransa nchini Cameroon ili kupafahamu, kuweka alama na kuzingatia idadi ndogo zaidi ya mazishi ya Waingereza katika eneo hilo.⁵³

Katika kujaribu kupunguza umbali kati ya ofisi yake kuu huko London na kazi zake, katika maeneo mengine IWGC ilianzisha vituo vya operesheni karibu na viwanja vya vita vya zamani. Wawakilishi katika vituo hivi walifanya kazi kama waamuzi kati ya IWGC na

⁵¹ TNA, CAB 24/199/48, 'Kumbukumbu ya Katibu wa Jimbo la Wakoloni, L.S. Amery, kuhusu malipo ambayo hayakulipwa kwa washiriki wa Kikosi cha Wafanyikazi wa Kijeshi, Juni 1925. Inaonekana kutokana na utoaji wa rekodi ambazo hazijakamilika na Ofisi ya Vita imemaanisha kuwa karibu robo tatu ya Wacyriot ambao walianguka kama sehemu ya Kikosi cha Wamakedonia - wanaume 149 - hawajapata maadhimisho ya jina. Shukrani zetu kwa Dkt Andrekos Varnava kwa kushirikisha habari hii. Tazama pia Varnava, Andrekos, *Serving the Empire in the Great War: The Cypriot Mule Corps, imperial loyalty and silenced memory* (Manchester: Manchester University Press, 2017).

⁵² Kuna matumaini kwamba orodha zinazozalishwa na Luteni-Kol. Oscar Watkins, ambaye alianzisha Ofisi ya Wafanyikazi wa Kijeshi na anaweza kuwa amerekodi vifo vya zaidi ya wanaume 42,000, na vifaa vingine vya kumbukumbu vinaweza kuwa vimewekwa ndani ya kumbukumbu za Kiafrika.

⁵³ Kwa maelezo, tazama CWGC/1/1/7/E/65.

mamlaka ya kikoloni au ya kigeni, wakifanya kazi kwa umbali mrefu zaidi kuliko wale wa maeneo ya Mapigano ya Magharibi. Pia walifanya kazi katika mazingira magumu zaidi na matokeo ya jambo hili ni kasi ndogo ya mawasiliano, uamuzi wao unaonekana kuwa wa mahesabu na si wa kuzuiliwa na kanuni ngumu zilizofuatwa huko Ulaya. Kama vile Fabian Ware alivyosema mnamo 1922 wakati alipokuwa akifanya kazi katika mazingira ya kikoloni, ikiwa Gavana alitaka aina ya maadhimisho ambayo hayawezi kabisa kuwa sawa na sera ya kawaida ya Tume, 'tunapaswa, kwa sababu nyingi, kutii matakwa na ushauri wao kama iwezekanavyo'.⁵⁴ Taarifa hii iliruhusu maafisa wa IWGC kutoka nje ya kanuni za kimsingi za shirika, jambo ambalo lilisababisha kutofautiana katika utumiaji wa sera na kushughulikia wafu. Mfano mmoja ulio wazi ni kumbukumbu ya Seychelles Carrier Corps. Kikosi hiki cha wanaume 791, kilichotokana na visiwa vyenye jumla ya takriban watu 24,000, kilipelekwa German East Africa (sasa Tanzania) mnamo 1916 na walipatwa na vifo 341. Kati yao, 290 walifariki Afrika Mashariki (kuna mmoja tu aliye na kaburi linalojulikana), 3 walifariki nchini India na 48 walikufa kutokana na magonjwa baada ya kurudi nyumbani mnamo Agosti 1917.⁵⁵ Mnamo Aprili 1926 IWGC ilikubali kutoa mawe ya makaburi kwa wale 48 waliozikwa huko Mont Fleuri huko Ushelisheli. Wakati huo huo, ilikubali kuweka kumbukumbu ndani ya makaburi hayo ili kuadhimisha, kwa jina, 289 ambao hawakuwa na makaburi yaliyojulikana ndani ya Afrika Mashariki. Tofauti na sera iliyowekwa na IWGC ya kuadhimisha wafu mahali walipokufa, mfano huu unaonyesha vitendo hivi - safari hii ili kumfurahisha gavana wa Ushelisheli ambaye aliona kuwa 'ukumbusho kama huo katika Afrika Mashariki hautawavutia wenyeji na labda haitawahi kuonekana na jamaa zake'.⁵⁶ Wahindi waliokumbukwa Basra hawakupewa makubaliano kama hayo, licha ya imani kwamba familia hazitatembelea na, mnamo 1924, kwamba Iraq

⁵⁴ CWGC/1/1/7/E/53, 'Barua: Fabian Ware kwa J.N. Cormack', 23 Juni 1922, pp. 35-6.

⁵⁵ Kaburi hilo linalojulikana lilikuwa Dar es Salaam, Pugu Road, Makaburi ya Kikristo ya 'Wenyeji'. Hakuna mawe ya makaburi yaliyowekwa juu ya makaburi haya kwani majeruhi wote waliadhimishwa kwa nambari kwenye skrini ya ukuta. Walakini, mnamo 1959, eneo hili lilionekana kuwa haliwezi kustahimilika na maafa haya sasa yanaadhimishwa kwenye Ukumbusho wa Barabara ya Pugu - tazama CWGC/2/2/1/425, *Mkutano wa Tume Namba 425*, 21 Mei 1959, pp. 9-10; <https://www.cwgc.org/find-records/find-war-dead/casualty-details/123962/%20LOUIS%20CHARLES/>. Watatu waliokufa nchini India walizikwa katika kaburi la Bombay (Sewri) na sasa wanaadhimishwa kwenye kumbukumbu ya Kirkee.

⁵⁶ CWGC/2/2/1/87, *Mkutano wa Tume Na.87*, 14 April 1926, p. 10.

ilikuwa "haifikiki kabisa", ilikuwa hatari na "haifai kwa jamaa wa kawaida" wa askari yeyote.⁵⁷

Lakini labda moja ya changamoto kubwa zaidi ya sera ya IWGC nje ya Ulaya ilikuwa jinsi ambavyo dini inavyoeleweka au fikra kuhusu ibada za mazishi ziliathiri wafu walivyoshughulikiwa. Katika taarifa ya umma ya Rudyard Kipling kuhusu mradi wa IWGC 1919 alibaini, 'katika mambo yote hayo miili ya askari...[wahindi] inavyoshughulikiwa itazingatia kabisa mwenendo wa dini zao'.⁵⁸ Mapema kabisa katika maoni ya shirika juu ya jinsi itakavyoshughulikia suala la wafu wa Himaya na kwa hivyo katika hatua hii hili lilihusu Jeshi la India na vifo upande wa mapigano wa Magharibi, bado inaangazia nia ya kutambua na kuheshimu njia tofauti ambazo dini zilishughulikia wafu wao. Kama ilivyosemwa awali, ni wazi kwamba wakuu katika IWGC pia waliendelea kuamini maamuzi haya mapana ya usawa katika kifo, na mwaka 1926, Ware anaposema kwamba lengo la Tume lilikuwa kwamba 'askari wote wa Himaya wanapaswa kuwa sawa'.⁵⁹ Maneno haya bado yalikuwa yameandikwa huku dini kuu za India ya Waingereza - Uhindu, Usingasinga na Uislamu - jambo lililoleta utata pale maneno kama 'sare' yalipotumiwa, kwani dini mbili kati ya hizi tatu zinaamini kuchoma moto kufuatia kifo. Katika kesi nyingi, hata hivyo, suala hili lilitatuliwa kwa kuanzishwa kumbukumbu za maiti waliounguzwa ambapo majina ya wafu yalikuwapo, lakini sio mifano yote ya aina hii inayochunguzwa.

Licha ya kuenea kwa imani ya Kiislamu na kazi kubwa za kimishenari zilizosambaa sehemu tofauti ili kuingiza Ukristo, utamaduni wa kidini katika bara zima la Afrika haukuwa sare na ulionyoka moja kwa moja. IWGC inajaribu kukidhi mahitaji ya imani katika bara hilo, au ukosefu wa imani unaoonekana, katika mazingira mengi imekuwa ikitumika kuhalalisha utofautishwaji, na hapa ndipo masuala makubwa yanakabiliwa. Kimsingi, sera hizi zinaweza kuelezewa kama jaribio la kutofautisha kati ya zile zinazoonekana kufuata dini zilizozoeleka, dini za kawaida au zile zinazotoka katika mila hizo, na zile zinazoonekana kufuatilia imani za 'kipagani' au kutokuwepo kwa dini kabisa.

⁵⁷ CWGC/1/1/7/E/77, 'Mhadhara umetolewa na Kanali Durham (Mkurugenzi wa Kazi)', 5 Mei 1924, pp. 14-16.

⁵⁸ Kipling, *The Graves of the Fallen*, p. 13.

⁵⁹ CWGC/2/2/1/88, *Mkutano wa Tume Na.88*, 12 Mei 1926, p. 8.

Mbali na haya kuwa mawazo ya IWGC tu, maoni haya yanaonekana kuwa na mizizi ndani ya sera za himaya. Kwa mfano, ingawa mfumo wa pensheni uliwekwa kwa wanaume walemavu au waliouawa wakati wa kutumikia Ofisi ya Wafanyakazi wa Kijeshi, msaada kwa wale wanaowategemea hao wanaume ulipatikana tu pale mtu huyo alipokuwa 'Mkristo muumini au Mwislamu'.⁶⁰

Sera hizi ambazo zina mizizi katika mradi wa himaya, ziliathiriwa na maoni ya kisasa ya maendeleo na ustaarabu - maoni ambayo yalikuwa yamefungwa ndani ya safu za ukabila na dini zilizounga mkono himaya. Ilikuwa kwa sababu hii ndiyo vitengo kama Kikosi cha West India, Kikosi cha British West Indies na vitengo vya watu 'waliochanganya' wa Afrika Kusini walizingatiwa kama 'Wazungu' badala ya 'wenyeji' machoni mwa watunga sera wa IWGC wa miaka ya 1920.⁶¹ Kutoka kwa makoloni yaliyodumu kwa muda mrefu na mila za Kikristo, wanaume hawa wangepokea aina ya uadhimisho wa majina kila ilipowezekana na, kwa hali hiyo, wengi walifurahia usawa mkubwa katika kifo kuliko walivyokuwa hai. Sera ya IWGC barani Afrika katika miaka ya 1920, hata hivyo, ilidhihirisha fikira pana za himaya kwa kuunda safu ya kuadhimisha ambayo ilitofautisha kibaguzi vikundi vya kikabila na dini tofauti. Ingawa shirika lilitafuta ushauri kutoka Ofisi ya India, Jeshi la India na utawala wa kikoloni wa India juu ya jinsi bora ya kukabiliana na wafu wa India, ilikuwa Afrika iliyowapa tatizo gumu zaidi. Ushauri uliotafutwa kutoka kwa wasimamizi wa kikoloni wa Uingereza na maafisa wa jeshi haukuchukua tahadhari au haukujali kabisa mila za kikabila zilizokuwa nyingi na tofauti, tena nyingi ambazo hazikuhusiana na kanuni za kidini zilizotambuliwa au kueleweka. Badala yake hawa walichukuliwa kama 'wapagani' au 'washenzi', hoja ambazo zilitumika kuunga mkono utofautishwaji wa wafu ambapo jamii husika zilisemekana kuwa hazijali - au hata zilikuwa na shuku ya - mazishi ya mtu binafsi na alama ya makaburi.

⁶⁰ TNA, CO 534/40/10, 'Kiambatanisho cha Agizo la Kulazimisha Na. 44, Pensheni za Kikosi cha Wafanyakazi wa Jeshi', 29 Agosti 1919, p. 52.

⁶¹ Tazama, kwa mfano, CWGC/1/1/9/D/28, 'Barua: Mkurugenzi wa Rekodi kwa Browne kuhusu "Askari wa Kienyeji wa Kiafrika" ambao "Wamepotea", 19 Mei 1924, p. 168; CWGC/1/1/9/D/29, 'Browne kwa Mkurugenzi wa Rekodi za Kuadhimisha Wenyeji katika Afrika Mashariki', 2 Oktoba 1925, pp. 28-9.

Ushahidi ufuatao uliotolewa kimsingi kutoka kwenye nyaraka za CWGC, unaonyesha mifano ambapo uadhimisho wa wafu wa vita ulivyotafautiana. Tofauti kutoka kwenye maoni yaliyoainishwa hapo awali kwa kiasi kikubwa zipo katika aina zifuatazo:

- Tume ilijua majina ya watu waliokufa na maeneo ya maziko, lakini yote yalitupiliwa mbali na iliamuliwa kuadhimishwa kwa kumbukumbu za kijumla, zisizokuwa na majina ya wahusika.
- Tume ilijua majina ya watu waliokufa na maeneo yao ya maziko, lakini maziko yalitupiliwa mbali na badala yake kumbukumbu za kijumla lilifanyika.
- Tume ilifahamu majina ya waliokufa lakini sio mahali pa kuzikwa; maadhimisho yalikuwa kwa mujibu wa nambari tu, na majina yalihifadhiwa katika usajili wa kumbukumbu.
- Tume haikujua majina ya watu waliokufa na maeneo yao ya maziko, hivyo iliamuliwa kuadhimishwa kwa kumbukumbu za kijumla, zisizokuwa na majina ya wahusika.

Kama itakavyoonyeshwa, sababu kadhaa zilisukuma maamuzi ya kuwatofautisha watu na vikundi tofauti katika kifo. Sababu zingine zililazimishwa kwa IWGC na zingine zilikuwa za kujitakia. Ingawa katika mifano fulani tofauti hizi zinaonyesha IWGC ikijitahidi kurekebisha hali mbaya, lakini kwingine inaonyesha kwamba shirika hilo lilihalalisha maamuzi ya kibaguzi kulingana na chuki za kidini, uwezekano wa ziara za uadhimisho kufanywa na jamaa na madai ya thamani ya kumbukumbu kwao - au ukosefu wa thamani - hivyo uadhimisho wa kawaida ungekuwa kwa mtu binafsi au kikundi. Ingawa katika idadi kubwa ya kesi haikufanya maamuzi haya kwa umoja, lakini ilihusika katika njia moja au nyingine, na maamuzi haya yanaiweka IWGC ndani ya mtandao wa Himaya ya Uingereza ambamo ubaguzi ulijaa. Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi majeruhi wengine walivyonyimwa uadhimisho wa jina pale ilipowezekana, na ni wangapi wengine ambao, kwa makusudi, walishughulikiwa tofauti na wafu wa Ulaya na pia tofauti na wafu Wazungu kwengine. Kwa kifupi, wanaume hawa walinyimwa usawa ambao IWGC ilikuwa imeahidi katika kifo.

iii. Uainishaji na mifano

Majina ya watu waliokufa na maeneo yao ya maziko hayakujulikana na Tume, lakini yote yalitupiliwa mbali hivyo iliamuliwa kuadhimishwa kwa kumbukumbu za kijumla, zisizokuwa na majina ya wahusika.

Katikati ya kanuni zilizotajwa za CWGC ni kwa kila majeruhi wa vita kuadhimishwa kwa jina katika jiwe la kaburi au ukumbusho wa waliopotea unaodumishwa milele. Utafiti huu wa awali umebainisha kesi ambapo IWGC haikufuata sera hii, na ingawa shirika limekuwa na maeneo ya mazishi na majina ya wafu lakini, kwa makusudi, hayakufanyiwa kazi.

Portuguese East Africa, ambayo sasa ni Msumbiji, ilikuwa eneo kubwa zaidi lisilo la Uingereza ndani ya Afrika Mashariki lililokuwa na idadi kubwa ya makaburi ya vita ya Himaya ya Uingereza kutoka Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Wakati jumla halisi iliyoripotiwa ilikuwa tofauti, idadi ya 'mazishi yaliyotambuliwa' yaliyoorodheshwa ndani ya Ripoti za Mwaka za IWGC za eneo hilo zimeshuka kutoka 510 mnamo 1924-5 hadi 277 mnamo 1925-6. 'Kutambuliwa' katika kesi hii haikumaanisha kupatikana, na kuna uwezekano kwamba habari hii ilitolewa hapo awali na Kitengo cha Usajili wa Makaburi, ambacho katika idadi kubwa ya kesi ililalamika kwamba makaburi ya Kiafrika hayajawekewa alama sawa wakati wa vita na haikuchukua hatua za kurekebisha hii.⁶² Inafikiriwa kwamba upunguzaji mkubwa unahusiana na idadi ya makaburi ambayo yangeweza kutambuliwa vyema wakati uamuzi ulipochukuliwa kati ya 1925 na 1926 ili kuacha makaburi yote yaliyotengwa kwa sababu ya umbali wao na ukweli kwamba mengi yalikuwa katika maeneo 'hatari na yanayotisha' katika nchi. Pale ambapo mahali pa mazishi palijulikana lakini sio eneo halisi la kaburi, hatimaye iliamuliwa kuachana na

⁶² CWGC/1/1/7/E/52, 'Meja George Evans, OC GRU Afrika ya Mashariki, kwa Mkurugenzi wa Kazi wa IWGC', 31 January 1920, pp. 73-4.

maeneo hayo.⁶³ Wale walioachwa nyuma walikuwa Waafrika au Wahindi na uamuzi huu ulijumuisha, ikiwa ni pamoja na mengine, mazishi katika makaburi yafuatayo.⁶⁴

Jedwali 3.1: Orodha ya makaburi yaliyotelekezwa katika Portuguese East Africa (sasa Msumbiji)

Makaburi	Wahindi	Cape Corps	Waafrika
Ankuabe	1		12
Balama			7
Bandari			50
Chinga			6
Inkinjiri			3
Koronje			3
Medo	3		5
Meza			6
Monapo			2
Mtarika		5	
Mwalia			1
Mwembe		2	
Namala			1
Namarika Rock			5
Nambari			4
Nampula	1		2
Natovi	1		17
Wanakote			5

Ingawa mazishi ya Wazungu katika maeneo haya kwa ujumla yalikuwa katika makaburi tofauti, hata hivyo, kwa kawaida waliunganishwa. Katika kesi za makaburi yaliyotajwa katika Jedwali 3.1, mazishi yote ya Uingereza yalizingatia kuwa katika makaburi ya kudumu na yalipewa mawe ya makaburi ya mtu binafsi.⁶⁵ Majeruhi wasio Wazungu ambao walibaki kwenye makaburi yaliyoungana waliadhimishwa katika kumbukumbu mbali mbali, ambazo asili yake ilitegemea kabila. Kwa mfano, wanajeshi watano wa Cape Corps waliozikwa kwenye Makaburi ya Mtarica waliadhimishwa, kwa majina, kwenye

⁶³ CWGC / 1/1/7 / E / 55, 'Ripoti ya F. Green kwa J.N. Cormack', 16 Novemba 1926, ukurasa wa 28-9; CWGC / 1/1/7 / E / 55.1, 'J.N. Cormack kwa Balozzi Mdogo wa Uingereza, Lourenco Marques', 17 Agosti 1925, ukurasa wa 100-1; CWGC / 1/1/7 / E / 55.1, 'Telegram kutoka kwa J.N. Cormack kwa Mkurugenzi wa Ujenzi', 5 Novemba 1926, p. 280; CWGC / 1/1/9 / D / 32, 'J.N. Cormack kwa Fabian Ware', 23 Novemba 1925, p. 157.

⁶⁴ Takwimu katika jedwali hili zimekusanywa kutoka vyanzo viwili: CWGC/1/1/7/E/55.1, 'J.N. Cormack kwa Balozzi Mdogo wa Uingereza Lourenco Marques', 22 Septemba 1922, pp. 56-61; tazama pia Ripoti za Usajili wa Kaburi katika CWGC/1/1/7/E/55, pp. 40-57.

⁶⁵ CWGC/1/1/7/E/55.1, 'Barua iliyoandikwa kwa mkono kwa J.N. Cormack', 26 Juni 1922, p. 55.

'kumbukumbu ya Kipling' iliyojengwa ndani ya Makaburi ya Pemba.⁶⁶ Hii inafungamana na fikra za IWGC, ambapo waliwachukulia hawa wa Waafrika ya Kusini kama Wazungu pale ilipowezekana. Mazishi ya Wahindi, isipokuwa wawili ambayo yaliachwa, yaliadhimishwa kwa nambari tu kwenye Ukumbusho wa Waingereza na Wahindi wa Dar es Salaam.⁶⁷ Kufuatana na kitendo cha maamuzi ya ajabu yaliyofanywa na tawala za kikoloni, wafu wa Afrika Magharibi waliadhimishwa kwa majina kwenye kumbukumbu zilizojengwa ndani ya nchi zao husika, wakati wafu wa Afrika Mashariki walikumbukwa katika kumbukumbu za jumla, bila jina huko Nairobi, Mombasa na Dar es Salaam. Kumbukumbu hizi za mwisho hazina usajili wenye majina ya wanajeshi wa Afrika Mashariki na wafuasi wanaokumbukwa, ikimaanisha majina yao, kwa sasa hayapo mahali popote.

Mchakato kama huo ulitokea ndani ya maeneo mengine ya Afrika Mashariki, ingawa kwa njia isiyo ya kawaida, kwani majina ya Waafrika waliojulikana kuwa wamezikwa ingawa maziko yao hayakutambuliwa kwa kuwa kwenye makaburi ambayo si ya kudumu waliachwa kwa njia hii wakati wa mchakato wa mkusanyiko. Ikifanywa kama njia ya kuimarisha mali ya Tume, na kwa hivyo kupunguza gharama zinazohusiana na kudumisha kabisa makaburi 3, 519 katika maeneo ya makaburi 295 yaliyoenea juu ya zaidi ya maili za mraba 500,000, maafisa wa IWGC katika miaka ya 1920 waliamini mchakato wa kukusanyia ulikuwa lazima. Kama matokeo ya sera hii na msimamo, rangi na dini viliamua uwezekano wa maiti kufufuliwa.⁶⁸ Kwa mfano, ripoti ya 1922 kususua Makaburi ya Mto Rufiji huko Tanganyika (sasa Tanzania) ilirekodi jumla ya mazishi 36.⁶⁹ Mnamo Oktoba 1924, mabaki ya askari 22 wa Uingereza, Afrika Kusini, Cape Corps na

⁶⁶ Ukumbusho wa Kipling au Ukumbusho Maalum ulitumiwa kutaja kaburi au makaburi ambayo hayakutambulika tena lakini ambayo zamani yalikuwa yanajulikana. Wanajeshi wawili wa Cape Corps huko Mwembe wanakumbukwa na kumbukumbu ya Kipling katika Makaburi ya Mji wa Mangochi, Malawi. Tazama <https://www.cwgc.org/find-records/find-war-dead/casualty-details/904884/ARTHUR%20COOK/#&gid=1&pid=3>; <https://www.cwgc.org/find-records/find-war-dead/casualty-details/904677/J%20VALENTINE/#&gid=1&pid=1>.

⁶⁷ Mnamo 2003 CWGC ilibadilisha vipande vya ujenzi kwenye ukumbusho huu ikiwa ni pamoja na majina ya Wahindi waliokufa, ambapo hapo awali ilikuwa imerekodi nambari iliyopotea kwa kitengo. Majina ya Wahindi yalikuwa yamehifadhiwa katika sajili peke yake hadi wakati huu.

⁶⁸ Kwa habari juu ya maamuzi ya mkusanyiko, tazama faili CWGC/1/1/7/E/56 na CWGC/1/1/7/E/57.

⁶⁹ Tazama jedwali katika CWGC/1/1/7/E/56, p. 9.

askari wa Kikosi cha West Indies cha Ungereza walifukuliwa na kukusanywa masalia na kupelekwa Makaburi ya Morogoro kutoka kwenye eneo hilo la awali, na hivyo kupaacha mahali hapo 'parudi kwenye maumbile asilia'. Haijulikani ikiwa yoyote ya mazishi 14 yaliyobaki yaliwahi kuwekwa alama, lakini kwa wakati huu Tume ilikuwa tayari imeamua kuwa askari wa Kiafrika katika mazingira haya "wataruhusiwa kutoweka" kwa sababu 'hakuna kumbukumbu zilizokuwa zimehifadhiwa za makaburi'.⁷⁰ Kwa sehemu kubwa, hii ilimaanisha kutokuwepo rekodi zozote - idadi kubwa haikujulikana kabisa baada ya vita - lakini pia ilienea hadi kwenye maeneo haya ambapo mazishi ya Waafrika waliotajwa kwa majina yalifahamika kuwapo lakini maeneo ndani ya makaburi hayakujulikana au yalionekana kama hayapatikani.

Tofauti pekee ya sera hii inapotumika kwa wafu wa Kiafrika katika makaburi ya nje ilikuwa ushahidi kwamba aliyejeruhiwa alifuata na kukubali dini inayofahamika mbele ya IWGC - kawaida Ukristo au Uislamu. Umuhimu wa hatua hii unaonekana kuwa na tofauti, wakati mwingine ulisababisha usawa kati ya watu, ingawa kwa ujumla hakukuwa a msimamo. Kwa mfano, katika 'muhtasari wa maamuzi ya Wenyeji na Wahindi' uliotumwa kwa Msajili wa IWGC mnamo tarehe 27 Julai 1925, marejeo yalifanywa kwa uamuzi wa Juni kuhusiana na mazishi katika Makaburi ya Kipenio huko Tanganyika (sasa Tanzania). Hapa Waafrika Kusini weusi wawili walipewa 'Kumbukumbu ya Kipling' huko Morogoro kwani walitambuliwa kama Wakristo. Mwafrika mwingine aliyezikwa huko Mpangas alifanyiwa kumbukumbu kama hiyo huko Morogoro.⁷¹ Inajulikana kuwa mazishi mengine ya Kiafrika yalikuwepo katika maeneo haya, lakini inafikirika tu kwamba waliruhusiwa 'kurudi kwenye maumbile asili', na maadhimisho yao kuhamishiwa na kuwa kumbukumbu ya jumla, ambayo haina jina.⁷² Makaburi ya Mto Rufiji, tena, yanaonyesha mfano wa kupendeza na unaojipinga kwani, mnamo Juni 1925, Msajili wa IWGC alimwandikia Mkurugenzi wa Rekodi akifahamisha kwamba Waafrika wawili waliobaki hapo

⁷⁰ CWGC / 1/1/7 / E / 57, 'Msajili wa Mkurugenzi wa Kumbukumbu kuhusu Kambi, Afrika Mashariki', 21 Juni 1923, uk. 16; CWGC/1/1/9/D/29, 'Mkurugenzi wa Rekodi kwa Msajili', 26 Juni 1925.

⁷¹ CWGC/1/1/9/D/29, 'Ripoti juu ya maamuzi ya Wenyeji na Wahindi', 27 Julai 1925, p. 18; CWGC/1/1/9/D/29, 'J.N. Cormack kwa Mkurugenzi wa Kumbukumbu kwenye Makaburi ya Kipenio', 19 Juni 1925, p. 20.

⁷² Tazama jedwali katika CWGC/1/1/7/E/56, pp. 6, 8.

wanaojulikana kama - 'Hospital Boy Zenzuriguiza' na 'Cape Boy William' - walijulikana kuwa Wakristo na aliuliza ikiwa Tawi la IWGC la Afrika Mashariki linaweza kuipata na kuzingatia miili yao. Kwa kujibu, Mkurugenzi wa Rekodi alipendekeza kwamba hatua yoyote isichukuliwe kwani, wakati dini yao ilikubalika, 'hatuwezi kuanza kutofautisha kwa msingi huo'.⁷³ Maeneo yao ya mazishi na majina yao, pamoja na yale ya dini zisizojulikana, zilitelekezwa na IWGC.

Katika baadhi ya makaburi ya kudumu, kuna mifano ya makaburi ya Waafrika kuachwa makusudi bila ya kuwekewa alama. Hii inaonekana katika Makaburi ya Wakristo ya Beira huko Portuguese East Africa (sasa Msumbiji), ambapo askari 18 wenye asili ya kienyeji walikuwa makaburi yao yametambuliwa kama ya 'Askari Wenyeji wa Kiafrika' lakini maelezo yao baadaye yalifutwa. Badala ya kuashiria makaburi haya binafsi, ilielekezwa kwamba watu hawa walipaswa kuadhimishwa katika Kumbukumbu ya Waafrika ya Dar es Salaam isiyo na majina.⁷⁴ Ni makaburi ya watu weupe tu wa Afrika Kusini na Wazungu ndiyo sasa yamebakia Beira. Vile vile, katika Makaburi ya Mjini Zomba Nyasaland (sasa Malawi), kuna askari wawili wa Kikosi cha Wenyeji cha Rhodesia ambao katika miaka ya 1920, walihesabiwa kama wamo katika makaburi kwa madhumuni ya takwimu tu, walitambulika kama "waliokosekana" kwa ajili ya maadhimisho.⁷⁵ Wakati makaburi ya Zomba hayakuwekewa alama, majina yalijulikana, lakini hayakuigingizwa kwenye usajili wa makaburini wala kwenye kumbukumbu. Katika mifano yote miwili, sababu za kutoweka mawe ya kaburi katika makaburi binafsi zinahusishwa na kanuni inayosema kwamba 'wenyeji' wa Kiafrika wanaozikwa kwenye makaburi ya kudumu wataadhimishwa kijumla kuliko kibinafsi.⁷⁶ Kwenye mfano wa Zomba, lakini mfananisho wake ambao unaweza

⁷³ CWGC/1/1/9/D/28, 'Msajili wa Mkurugenzi wa Kumbukumbu kwenye Makaburi ya Mto Rufiji', 27 Juni 1925, p. 270; CWGC/1/1/9/D/29, 'Mkurugenzi wa Kumbukumbu kwa Msajili kwenye Makaburi ya Mto Rufiji', 30 Juni 1925, p. 23.

⁷⁴ Inaonekana maelezo machache sana yalijulikana juu ya majeruhi hawa na kazi zao, jambo ambalo linaweza kuwa limeathiri uamuzi wa kuwakumbuka kwa pamoja. Tazama usajili wa Makaburi katika <https://www.cwgc.org/find-records/find-war-dead/casualty-details/904788/%20MIR%20ZAMAN/#&gid=1&pid=4>.

⁷⁵ Tazama Ripoti ya Usajili wa Kaburi kwenye <https://www.cwgc.org/find-records/find-war-dead/casualty-details/6000539/JULIUS%20BARTHEL/#&gid=1&pid=1>.

⁷⁶ CWGC/1/1/7/E/56, 'Sera inayopendekezwa kwa Wenyeji wa Kiafrika', c.1921-22, pp. 49-50.

kutumika hata kwengine, ni kwamba, mwaka 1925 ilionekana na Mkurugenzi wa Kumbukumbu kwamba:

N.K.M [Naibu Katibu Mkuu, Arthur Browne] ana maoni kwamba kikosi cha Cape Boys kinapaswa kupewa heshima zote kama Askari wa Kiingereza, lakini kuhusu askari wa Kiafrika, ambao wangedhimishwa na Kumbukumbu fulani za Pamoja, mawe ya kaburini hayapaswi kujengwa, isipokuwa kama tumelazimika kufanya hivyo, na tusichukuwe jukumu la kutafuta ili kutambua.⁷⁷

Kwa wale waliozikwa ndani ya Beira, kumbukumbu ikiwa ni pamoja na majina yao iliwekwa kwenye Makaburi ya Pemba mnamo 2019. Watu hao wawili waliozikwa Zomba ni miongoni mwa kesi mpya ambazo ziligunduliwa na kamati hii na hivyo zinasubiri utaratibu kama huo. Wanavyoona IWGC mwaka 1920, vifo vyote hivi viliadhimishwa kwa pamoja, kwenye kumbukumbu zisizo na majina zilizoengwa kote Afrika Mashariki.

Majina ya waliokufa na maeneo yao ya kuzikiwa yalijulikana na Tume, lakini maeneo ya kuzikiwa yalitelekezwa na badala yake kuwekwa kumbukumbu za pamoja za uwakilishi.

Katika visa vingi, IWGC haijawahi kujua maeneo ya mazishi ya majeruhi 500,000 wa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Hatimaye ilihesabiwa kwamba wamepotea. Kwa sehemu kubwa, hii ilikuwa ni kwa sababu waliokufa kamwe hawakufanyiwa mazishi rasmi au yaliyosajiliwa. Au maeneo ya mazishi yaliharibiwa au kupotea wakati wa vita. Hata hivyo, kulikuwa na wakati ambapo makaburi yaliyojulikana yalifanywa kama vile 'yamepotea' ambayo ni kama kusema yalipotezwa kwa makusudi, na kuyaweka katika kitengo hicho hicho kama makaburi mengi yasiyo ya Wazungu barani Afrika. Kunaonekana maelezo tofauti ya aina mbili katika mamlaka hii ya IWGC. Ya kwanza ilikuwa ujenzi wa kumbukumbu za pamoja kwenye makaburi ya kudumu kuliko ya kuwajengea mawe ya kaburi binafsi kwa wale waliokuwa wameshazikwa. Ya pili ilipewa jina la maadhimisho ya kuwakilisha kumbukumbu za umma, ingawa makaburi ya watu binafsi yalikuwa

⁷⁷ CWGC/1/1/9/D/29, 'Mkurugenzi wa Ujenzi kwa Msajili wa Makaburi ya Zomba', 22 Juni 1925, p. 21.

yanajulikana – vuguvugu la kishindo hasa Afrika Magharibi, ambalo lilisukumwa kwa kiasi kikubwa na mamlaka ya kikoloni.

Tofauti 1 - Kuadhimisha kijumla katika makaburi ya kudumu

Sera hii kwa ujumla ilitumika kwa mazishi ya Wahindi huko Afrika Mashariki, Misri na Palestina. Haya yalikuwa mapambano katika medani za vita ambamo Jeshi la Kihindi lilikuwa linashiriki kikamilifu, kupoteza zaidi ya vifo 8,000 kwa ujumla. Tangu kuanzishwa kwake, IWGC ilikuwa imetafuta sera inayofaa ya matibabu ya wafu wa India ambayo ingeheshimu dini anuwai za wale waliopigana. Hakika, katika mkutano wa pili wa Tume Februari 1918, Waziri wa Mambo ya Nchi wa India, Bwana Islington, alijenga hoja kwamba 'haipaswi kuwepo hali ya kutafautiana kabisa baina ya makaburi ya Wahindi na yale ya Wakristo'.⁷⁸ Kama matokeo, baada ya majadiliano na Ofisi ya India, mnamo Septemba 1920 ilikubaliwa kuwa mazishi yote ya Wahindi ndani ya Ulaya yangeadhimishwa 'kwa mawe ya makaburi binafsi ambapo makaburi yaliyotambuliwa yalikuwapo'.⁷⁹ Walakini, mnamo Desemba 1920, IWGC ilifahamishwa na Jenerali Bwana Herbert Vaughan Cox wa Jeshi la India kwamba, ndani ya Misri, 'kusiwe na mawe ya kaburi juu ya makaburi ya Wahindi bali ukumbusho wa jumla unaoashiria ardhi ambayo Wahindi walikuwa wamezikwa'.⁸⁰

Jenerali Cox alikuwa afisa katika jeshi la India tangu miaka ya 1880 na alikuwa akiamuru kikosi cha Wahindi wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia huko Arabuni, Misri na Gallipoli. Mwaka 1917 aliteuliwa kuwa katibu wa idara ya kijeshi katika Mamlaka ya India, na kama mwakilishi wa Waziri wa Mambo ya Nchi kwa India alikuwa amehusika na IWGC kutoka kuanzishwa kwake. Kwa amri ya IWGC, mwezi Novemba na Desemba 1920 Cox alikuwa amezuru maeneo ya makaburi saba ya Wahindi nchini Misri - Alexandria, Abbasiya, Ismailia, Suez, Port Said na mawili huko Kantara, kwa pamoja kuadhimisha zaidi ya mazishi 700 au uchomwaji wa miili – kutoa mapendekezo kuhusu namna sahihi ya maadhimisho hayo. Kulingana na mapendekezo ya Baraza la India, alishauri kwamba

⁷⁸ CWGC/2/2/1/2, *Mkutano wa Tume Na.2*, 20 November 1917.

⁷⁹ CWGC/2/2/1/26, *Mkutano wa Tume Na.26*, 21 Septemba 1920, uk. 6-7; CWGC/1/1/7/E/56, 'makaburi ya Wahindi huko Makedonia', 15 Desemba 1921, p. 62

⁸⁰ CWGC/2/2/1/28, *Mkutano wa Tume Na.28*, 20 Desemba 1920, p. 4.

majina tu yanahitajika kuorodheshwa kwa kuitwa jina moja moja, kwa vile Waislamu na Wahindu 'hawakuweka umuhimu' wowote katika kuorodhesha majina ya waliokufa kwenye kaburi la mtu binafsi. Katika maeneo mawili tu – Makaburi ya Wahindi ya Alexandria (yenye makaburi 112 ya Waislamu) na Port Said (yenye makaburi 24 ya Waislamu) – alitoa taarifa kwamba utambulisho wa makaburi hayo ulikuwa 'kwa ujumla hauwezekani'.⁸¹ Kufuatia mapendekezo haya, mnamo Agosti 1921 IWGC ilikubali kwamba makaburi ya Wahindi nchini Misri na Palestina hayatapokea mawe ya mtu binafsi, na kwamba badala yake 'katika kila maeneo ya makaburi ambapo makaburi yaliyotambuliwa yapo' kumbukumbu ya kijumla yenye majina yao itajengwa.⁸² Hata hivyo, kama Jedwali A5 ndani ya Kiambatisho cha 1 inavyoonyesha, wakati kumbukumbu hizi za makaburi zilipojengwa, majina ya Wahindi waliokufa yalijumuishwa tu katika usajili wa makaburi, kwani kumbukumbu zenyewe zilijumuisha idadi tu ya wale waliozikwa karibu.

Ingawa alikuwa akitegemea mapendekezo ya Baraza la India, Cox alibaki na ushawishi mkubwa katika mchakato huu, kwa vile IWGC na kamati yake nchini Misri ilimwachia yeye majukumu yote.⁸³ Japo Cox alitafuta ushauri kutoka kwa afisa wa Kisingasinga na Dogra kuhusu utaratibu bora kwa wale wanaochochomwa moto, na bila ya shaka alikuwa amebobea kwa mila na desturi zao kutokana na uzoefu wake wa muda mrefu, kutokujengwa kwa mawe kwenye makaburi kulitokana na uelewa wake mahsusi wa Wangereza kuhusu desturi za mazishi ya Wahindi, bila ushahidi wowote wa mashauriano. Kwa hakika, kamati iliyoanzishwa kusimamia kuwa wakala wa IWGC nchini Misri ulikuwa na wawakilishi wa Kiingereza tu – wanne waliotoka idara mbalimbali za serikali na maafisa wa jeshi wawili.⁸⁴ Ingawa sera ya IWGC daima itahitajika kuongozwa na mahitaji ya walio

⁸¹ CWGC/1/1/9/D/12, 'Ripoti ya Jenerali Cox kwa Katibu Mkuu wa IWGC', 30 Desemba 1920, pp. 36-40; CWGC/1/1/7/E/56, 'Dondoo kutoka kwa Dakika za Mkutano wa Kumi na tano wa Kamati ya Makaburi ya Vita vya Anglo-Misri', 29 Novemba 1920, p. 60.

⁸² CWGC/2/2/1/36, *Mkutano wa Tume Na.36*, 1921, pp. 2-3.

⁸³ CWGC/2/2/1/27, *Mkutano wa Tume Na. 27*, 13 Oktoba 1920, uk. 2; CWGC/1/1/9/D/12, 'Ripoti ya General Cox', p. 40.

⁸⁴ Wajumbe wa Kamati hiyo mnamo Desemba 1920, wakati Cox alipoainisha ripoti yake, walikuwa Bw. J. Langley, Bw. C. de Cosson, Dk W. Hastings, Bw. Holden, Meja F. Athill na Meja R. Hilson. Wanne wa kwanza walihusika katika kamati ya kwanza ya Anglo-Egyptian, iliyoanzishwa mwaka 1918, ambayo pia ilikuwa na mjumbe Mkurugenzi Msaidizi wa DGRE, Tawi la Mashariki, Meja Palmer, angalia CWGC/2/2/1/3, *Mkutano wa Tume Na.3*, 24 Julai 1918, p. 1; for 1920 composition, tazama CWGC/2/2/1/28, *Mkutano wa Tume Na.28*, 20 Desemba 1920, pp. 3-5.

wengi badala ya mahitaji ya mtu binafsi, inatia shauku kuona kwamba kuna hata ushahidi wa kuonyesha kwamba baadhi ya watu wa madhehebu ya Singasinga walikuwa tayari hata kuepuka kuchomwa ikiwa mazishi yangeweka mawe katika makaburi na kufanya madhimisho ya kila mtu binafsi.⁸⁵ Hata hivyo, ingawa baadhi yao wasingetaka hivyo, maadhimisho ya kijumla badala ya maadhimisho ya mtu binafsi yalikuwa ndo sera ilokubalika ya IWGC kwa ajili ya Wahindi wote, bila kujali dini, nje ya Ulaya.⁸⁶ Hii iliathiriwa na imani kwamba Wahindi hawangefanya ziara za maadhimisho kwa maeneo haya kama vile wangeluweza ulaya. Lakini inawezekana azma ya kupunguza gharama kwenye serikali ya Waingereza huko India, ambayo mara kwa mara ilifanya bidii na IWGC kutafuta njia za kupunguza mzigo huu.

Katika baadhi ya hali, utaratibu kama huo ulipitishwa kwa ajili ya makaburi ya Waafrika yaliyopo kwenye maeneo ya makaburi ya kudumu, ambayo mapendekezo zaidi yalitolewa, pia inawezekana kati ya 1921-2. Kama ilivyo kwa makaburi ya Wahindi, pale ambapo makaburi ya Waafrika yalikuwa ndani ya maeneo ya kudumu ya makaburi yaliyochaguliwa, makaburi haya yangewekwa pamoja na kuwekwa alama za pamoja – isipokuwa kwa makaburi mawili ambayo ni ya 'Wenyeji wa Kikristo' na vikosi vya Cape Corps na vya British West Indies Regiment (BWIR). Makaburi haya yangepaswa kuchukuliwa kama ya Wazungu. Ni muhimu kutambua, hata hivyo, kwamba hata tofauti hizi hazikutumika kwa usawa. Kwa mfano, katika Makaburi ya Morogoro huko Tanganyika (sasa Tanzania), makaburi yaliyowekwa alama ya askari 49 na wafuasi katika kieneo cha 'Wenyeji wa Kikristo' – yakiwemo makaburi mawili ya Cape Corps na jengine moja kwa askari wa BWIR – yalikuwa 'yameondolewa kabisa'.⁸⁷ Wakati huo huo pendekezo lilikuwa limefanywa 'kimya kimya' kuweka alama kwa kujengea mawe katika makaburi binafsi ya

⁸⁵ Tazama Basu, Shrabani, *For King and Another Country, Indian soldiers on the Western Front 1914–18* (London: Bloomsbury, 2015).

⁸⁶ CWGC/1/1/7/E/56, 'Mapendekezo ya Maziko ya Kihindi', c.1921–22, p. 48.

⁸⁷ Kati ya idadi hii, 48 walitambuliwa na kutajwa. Neno 'kuondolewa kabisa' lilitumiwa na IWGC kuelezea jinsi kaburi lilivyokuwa limekanyagwa kwa hivyo halikuonekana tena. Katika kesi zingine, hii ilifanywa na jeshi au IWGC, wao waliona kwamba wanalinda kaburi kutokana na kuchafuliwa ambapo ilionekana kuwa hatari mara moja au mwishowe haiwezekani kutunza. Shughuli hii ilijulikana kutokea katika hali nyengine katika Afrika Mashariki, Persia, Mesopotamia na kando ya Mpaka wa Kaskazini Magharibi mwa India. Tazama, kwa mfano, CWGC/2/2/1/57, *Mkutano wa Tume Na.57*, 18 Julai 1923, pp. 8-9.

watu watano ambao waliaminika kuwa ni Wakristo, hii walighairi maana takribani wote waliozikwa katika sehemu hiyo walithibitishwa kuwa hivyo.⁸⁸ Badala yake, bila kujali sera maalum kuhusika na dini au kitengo, hakuna mawe kwa mtu binafsi yaliyoweka kwa maiti hawa ndani ya sehemu hii ya makaburi na maadhimisho yalijengewa kwa pamoja kwa kupitia vibao.⁸⁹ Zaidi ya hawa wengine 16 BWIR na maiti 59 wa Cape Corps walikuwa tayari washazikwa ndani ya makaburi katika kitengo cha sehemu kubwa ya Wakristo badala ya sehemu ya 'wenyeji' na hapa waliwekewa mawe katika makaburi ya kibinafsi, sambamba na sera ya kawaida ya IWGC.

Sera zilizokubalika pia ziliamua kwamba makaburi ya Waafrika nje ya maeneo ya makaburi ya kudumu yangeweza kustahili kufikiriwa kufufuliwa kwa kuwaleta pamoja kwa uhamisho ikiwa watathibitishwa kwamba ni waumini wa Kikristo au Kiislamu. Ili kujikinga dhidi ya 'kuamsha ushirikina wa kienyeji', iliamuliwa kwamba masalia ya wanajeshi wengine wote wa Kiafrika na wapagazi hawataingiliwa, na ardhi ambayo walizikiwa itaruhusiwa kurejea katika hali yake ya asili haraka iwezekanavyo. Huko Afrika Mashariki, minara ya kumbukumbu kwa watu hawa hapo awali yalipangwa kwa ajili ya Nairobi, Mombasa, Kampala, Dar es Salaam na Zomba, 'kusanifiwa na kuandikwa ili iweze kupata hadhi ya wazi kwa Waafrika wote wenyeji, ikiwa ni pamoja na Wapagazi, ambao walitoa huduma kwa Washirika wa vita na wakafa vitani'.⁹⁰ Wakati sera hizi hazikutumika kwa usawa, zinazungumzia mbinu za kijumla zilizopitishwa na IWGC, Afrika Mashariki na Mashariki ya Kati katika miaka ya 1920, ambayo ushahidi wake upo wazi.

Tofauti 2 - Kuadhimisha kijumla katika makaburi ya kudumu

Katika mkutano wa 75 wa Tume mnamo Machi 1925, Fabian Ware alisema kwamba kulikuwa na makaburi 109 huko Somaliland ya Uingereza ambayo yalihatiji tahadhari:

⁸⁸ CWGC/1/1/9/D/29, 'Ripoti ya sheria kwa maziko ya Wahindi na Wenyeji', 27 Julai 1925, p. 18.

⁸⁹ CWGC/1/1/7/E/56, 'Ripoti ya Mkurugenzi wa Kazi kwa Mshauri wa Fedha Ujenzi Afrika Mashariki, 1st Programme', 16 Agosti 1922, pp. 21-6; CWGC/1/1/7/E/56, 'Mapendekezo ya Maziko ya wenyeji Waafrika', c.1921-2, pp. 49-50; tazama pia Ripoti ya Usajili wa makaburi hapa <https://www.cwgc.org/find-records/find-war-dead/casualty-details/124552/PIET%20MOTLAKOANE/#&gid=1&pid=1>.

⁹⁰ CWGC/1/1/7/E/56, 'Mapendekezo ya Maziko ya wenyeji Waafrika', c.1921-22, pp. 49-50.

Wazungu 2, Wasomali 32 na Wahindi 75. Wazungu wangewekewa mawe katika makaburi ya kibinafsi, lakini kwa Wasomali na Wahindi:

Kaimu Gavana alichukulia kuwa haifai kujengea mawe sehemu ya kichwani mwa makaburi ya Wasomali kutokana na mawazo ya kibaguzi ya kidini. Sababu hiyo hiyo ilitumika kwa ajili ya makaburi ya Wahindi huko Somaliland, ambao wote walikuwa Waislamu na Wahindu kama ilivyotarajiwa walikuwa wamechomwa moto. Makaburi yalitawanyika kote katika maeneo ya makaburi kwenye Himaya ya mkoloni na hakuna ambayo yaliweza kufanyiwa ukarabati ipasavyo. Hali ya hewa pia iliaminika kuwa haingefaa kwa ujengaji wa mawe kwenye makaburi.

Kwa sababu hizi, kaimu gavana alipendekeza kwamba Wahindi na Wasomali waadhimishwe kwenye vipande vya mawe ambavyo vingejengewa katika ngome huko Burao. Bwana Alexander Cobbe, anayewakilisha Waziri wa Nchi wa India, aliongeza kuwa 'alidhani wanapaswa kukubali maoni ya gavana wa eneo hilo...[kama] hali nchini ilikuwa ngumu'. Kwa kuungwa mkono na Makamishna wa IWGC, mbinu hii iliidhinishwa.⁹¹ Hivyo, ingawa Wahindi wengi na Wasomali walizikwa katika makaburi yaliyokuwa na alama iliyotambulika, iliamuliwa kutoweka mawe binafsi.⁹² Hadi hii leo, kuna majina 114 ambayo kwa sasa yamesajiliwa kwenye hifadhidata ya Tume kwa ajili ya Somalia: watano kati ya hao ni maafisa wa Kiingereza na makaburi yao yaliwekewa alama. Yaliyobakia yaliadhimishwa katika Kumbukumbu ya Berbera

Katika nchi ya Gold Coast (ambayo sasa ni Ghana), Nigeria na Sierra Leone, ambazo zilikuwa na mazishi takribani 600 kwa pamoja, hakuna kifo cha Mwafrika wakati wa Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia kilichoadhimishwa kwa kuwekewa jiwe kaburini. IWGC haikuwa na maafisa katika eneo la Afrika Magharibi na badala yake walifanya kazi kupitia tawala za mitaa, hatimaye kupitisha sera ambayo ilihisi kwamba 'makaburi yote ya wazungu yanayojulikana Afrika Magharibi yatajengewa mawe kichwani mwa kaburi. Yale

⁹¹ CWGC/2/2/1/75, *Commission Meeting* Na.75, 11 March 1925, pp. 9–10.

⁹²Tazama, kwa mfano, <https://www.cwgc.org/find-records/find-war-dead/casualty-details/1419807/%20NUR%20MUHAMMAD/#&gid=2&pid=1>; <https://www.cwgc.org/find-records/find-war-dead/casualty-details/1419827/%20ADAN%20MUHAMMAD/#&gid=2&pid=1>.

yote ya wenyeji (iwe yamezikwa katika makaburi yanayojulikana au la) yataadhimishwa kwenye kumbukumbu'.⁹³ Uamuzi huu ulitokana na mambo tofauti lakini, hususan, kwa kiasi kikubwa uliainishwa na utawala wa kikoloni wa Afrika Magharibi. Moja ya masuala muhimu zaidi yalioshinikiza Tume ilikuwa kwamba idadi kubwa ya minara ya kumbukumbu – manne nchini Nigeria na moja katika Gold Coast - hayakujengwa na shirika hilo. Kumbukumbu hizi za vitengo, zilizolipiwa kupitia michango ya umma na kujengwa na serikali za kikoloni, zinaadhimisha kwa majina askari wa Kikosi cha Nigeria na Kikosi cha Gold Coast, bila kujali kama walikuwa na mazishi yaliyotambulikana. Tofauti na utata ulioonekana katika njia ya kuweka kumbukumbu ni mambo mapya kwa sababu katika kesi zote hizi mbili, ni magavana ambao walipinga kuwekwa kwa mawe sehmu ya vichwa katika makaburi ya watu binafsi, na ilikuwa ni matakwa yao ambayo yalitungwa kinyume na kanuni za IWGC.

Takwimu za IWGC kuanzia Aprili 1923 zinaonyesha kulikuwa na mazishi ya 'maafisa weupe' 7 na 'wenyeji' 108 hapo Gold Coast. Ripoti ya baadaye iliibua idadi kamili ya mazishi ya Waingereza kufikia hadi kumi, ambapo kila kaburi moja sasa limewekewa alama ya Tume katika jiwe la kaburi.⁹⁴ Kwa upande mwingine, kila moja ya vifo 108 vya Waafrika viliadhimishwa kwa jina kwenye eneo la kumbukumbu za Kumasi. Ingawa hapo awali, IWGC iliishinikiza mamlaka ya Gold Coast kufikiria kuashiria makaburi hayo ya Waafrika ambayo yalifikiriwa kwamba yametambuliwa. Utaratibu huu ulianza Agosti 1922 wakati Gavana wa Gold Coast, F.G. Guggisberg, alipoifahamisha Ofisi ya Kikoloni kwamba kumbukumbu kuu kwa ajili ya askari wa Kikosi cha Gold Coast waliokufa, ulipangwa kuwa Kumasi. Uamuzi huu ulidaiwa kuendana na tangazo la Juni 1921 lililosambazwa katika mamlaka ya Uingereza na kusainiwa na Winston Churchill, Waziri wa Mambo ya Nchi kwa makoloni kwa wakati huo. Lilitumwa kwa niaba ya IWGC na kunakili maudhui yake mengi kutokana na mawasiliano ya awali yaliyotumwa kwenye Ofisi ya Kikoloni na Arthur Browne. Waraka huu ulieleza kwamba kumbukumbu za pamoja badala ya zile za watu

⁹³ CWGC/1/1/7/E/62, 'Browne kwa Kapten King kuhusu Afrika Magharibi', 4 Septemba 1930, pp. 110-11.

⁹⁴ CWGC/1/1/7/E/67, 'Memo: P.A.S., Arthur Browne', 4 April 1923, p. 4; CWGC/1/1/7/E/62, 'Summary of Graves', 6 December 1929, p. 101

binafsi zinapaswa kujengwa kwa Waafrika barani Afrika.⁹⁵ Licha ya jukumu lake katika kupeleka ujumbe, Browne alimjibu Guggisberg akieleza kuwa wakati 'pendekezo hili linaendana na mujibu wa mazoea ya Tume hii lakini katika maeneo mengine ya Afrika ambako makaburi ya wenyeji hayana kumbukumbu, lakini kadiri idadi ya makaburi ilivyotambulika, kumeonekana uwepo wa swali moja katika Maeneo ya Gold Coast na linahitaji kuzingatiwa...na Gavana'.⁹⁶

Shinikizo la kufikiria upya mwelekeo huko Gold Coast linaonekana kuwa la kipekee na inawezekana zaidi lilikusika na kukosekana na maendeleo yalokwisha fanyika kule. Hii imetafautiana kiasi fulani na maingiliano na Nigeria, ambapo gavana, Bwana Hugh Clifford, alikuwa tayari anasimamia ujenzi wa kumbukumbu za vikosi.⁹⁷ Wakati Browne alipomuandikia Clifford mwaka 1923 akielezea majukumu ya IWGC na kufafanua chaguzi tofauti za maadhimisho ya kibinafsi na pia ya pamoja kwa ajili ya Waafrika 294 waliozikwa nchini Nigeria, Gavana huyo aling'ang'ania kwamba hilo la mwisho litatosha.⁹⁸ Akiwa na uwezo wa kubadilisha uamuzi huo huko Gold Coast, Browne aliandaa mkutano na Guggisberg jijini London tarehe 18 Mei 1923, ambapo Guisberg alidai kwamba:

mwenyeji wa kawaida wa Gold Coast hangeelewa au kuthamini jiwe kaburini. Na kwamba pendekezo la awali la O.C. Troops, kwamba: - sanamu la askari linalowakilisha kikosi cha Gold Coast - lilikuwa ni pendekezo la busara zaidi. Kumbukumbu kama hiyo ingeeleweka na kuthaminiwa sana na makabila ambayo miongoni mwao wengi wa askari wa kikosi walijajiriwa.

⁹⁵ CWGC/1/1/7/E/67, 'Letter: F.G. Guggisberg to Winston Churchill', 9 August 1922, p. 81; for the Colonial Office despatch and Browne's influence on it, see, CWGC/1/1/7/A/10, pp. 17-18, 28-9.

⁹⁶ CWGC/1/1/7/E/67, 'Letter: Browne to the Under-Secretary of State, Colonial Office', 5 April 1923, p. 89.

⁹⁷ CWGC/1/1/7/E/63, 'Report: Graves in Nigeria', 27 August 1924, pp. 169-72.

⁹⁸ CWGC/1/1/7/E/63, 'Barua: Browne kwa Gavana wa Nigeria', 12 Aprili 1923, pp. 128-32; kwa kujibu, IWGC iliarifiwa kuwa kama kumbukumbu pamoja na majina yalikuwa tayari yanajengwa huko Zaria, Lokoja, Ibadan na Calabar, 'ujenzi wa kumbukumbu binafsi kwa askari wa Kiafrika sio lazima' - CWGC/1/1/7/E/63, 'Barua: Serikali ya Nigeria kwa IWGC', 11 Januari 1924, pp. 140-3. Kati ya Wanaijeria 294 waliojulikana kuzikwa ndani ya Nigeria, 114 walizikwa katika makaburi 18, na 180 walizikwa katika maeneo 54 ya makaburi, angalia CWGC/1/1/7/E/63, 'Msajili kwa Mkurugenzi wa Rekodi kwenye Makaburi nchini Nigeria', 24 Desemba 1925, p. 243.

Katika jibu linaloonyesha kile ambacho alibashiria kama kuona mbali, ingawa kiukweli ni kwamba ilikuwa wazi uamuzi huu kimsingi ulitokana na ubaguzi wa kikabila wa wakati ule, Browne alisema kwamba, 'labda katika muda wa miaka mia mbili au mia tatu ijayo, wakati wenyeji wamefikia hatua ya kiwango cha juu cha ustaarabu, inawezekana wakafurahia kuona kwamba mawe yalikuwa yamejengewa kwenye makaburi ya wenyeji na kwamba askari wa kienyeji walikuwa wametendewa haki sawa na askari wenzao wa kizungu'. Hata hivyo, kama Clifford, Guggisberg pia aliridhika na wazo la maadhimisho ya pamoja.⁹⁹

Licha ya Browne kujitahidi zaidi, mnamo Juni 1925 Tume ilipokea ripoti ikisema kuwa maeneo mengi ya mazishi ya 'wenyeji' huko Gold Coast hayatambulikani tena.¹⁰⁰ Kwa vile Kumbukumbu za Kumasi zilikubalika kama aina iliyotosheleza kwa maadhimisho, maeneo hayo ya makaburi yaliyobaki yaliachwa bila alama na majina ya maadhimisho hayo yaliamishwa kwenye kumbukumbu za Usajili wa Kumasi.¹⁰¹ Sababu ya hili jambo, kama vile Arthur Browne alivyoelezea mnamo Novemba 1925, ilikuwa kwamba kuendelea kuweka majina yao katika usajili wa makaburi, 'itakuwa ni kazi bure ya kuwashtuwa katika ukweli kwamba sisi tumepuuza kuadhimisha kwa kuweka jiwe la kaburi'.¹⁰² Utaratibu huu unaonekana kuwa ulileta ufanisi sana, kwa vile ilipofikia mwaka 1930 hakuna mazishi ya Kiafrika yaliyowekwa katika kumbukumbu za Gold Coast.¹⁰³ La kushangaza ni kwamba mpango huu haukuonekana kufanyika nchini Nigeria, ambapo mnamo Juni 1930 Mkurugenzi wa Ujenzi aliuliza kama anapaswa kuweka alama za Wanaijeria 5 waliozikwa katika makaburi ya Kaduna na 9 (kati ya jumla ya 29) ambao bado

⁹⁹ CWGC/1/1/7/E/67, 'Mahojiano ya Browne na Bwana Frederick Guggisberg', 18 Mei 1923, p. 95.

¹⁰⁰ CWGC/1/1/7/E/67, 'Barua: Browne kwa Gavana wa Gold Coast', 29 Mei 1923, pp. 96–100; CWGC/1/1/7/E/67, 'Barua: Mkurugenzi wa Rekodi kwa Browne kuhusu Makaburi Gold Coast', 9 Juni 1925, p. 123.

¹⁰¹ Ona CWGC/1/1/7/E/67, 'Mawasiliano kati ya Mkurugenzi wa Rekodi na M.M. Tawi (Kumbukumbu kwa Tawi lililokosekana)', 29 Aprili 1929 - 1 Mei 1929, pp. 191–7; CWGC/1/1/7/E/62, 'Mkurugenzi wa Rekodi za Browne kwenye Kumbukumbu za Afrika Magharibi', 2 Oktoba 1928, pp. 47–9.

¹⁰² CWGC/1/1/7/E/67, 'Barua: Browne kwa Mkurugenzi wa Rekodi', 24 Novemba 1925, p. 130.

¹⁰³ CWGC/1/1/7/E/62, 'Muhtasari wa Makaburi', pp. 96–103.

wanatambulika katika makaburi ya Ikoyi.¹⁰⁴ Kwa vile majina yao yalikuwa yameshatumwa zamani kwenye kumbukumbu za maadhimisho Ibadan kwa mujibu wa taratibu za kienyeji, uchunguzi huu haukuendelezwa zaidi.

IWGC haikuwa na msukumo wa aina za maadhimisho ambayo hatimaye yalifanywa nchini Somalia na Afrika Magharibi. Ingawa iliweka wazi maamuzi yake Afrika ya Mashariki, ni wazi kwamba Tume ilitarajia mamlaka za serikali husika nchini Nigeria na Gold Coast kuweka alama kwenye makaburi ya askari wao wote waliokufa –Waafrika na Wazungu – kwani walionekana 'kutambulika katika kila hali'. Hata hivyo, sambamba na maelekezo ya Fabian Ware kwa Tume kufungamana na mahitaji au tamaa za utawala wa kikoloni, IWGC ilifanya kazi kinyume na kanuni zake zenyewe na kujihusisha dhidi ya msimamo wake katika uamuzi wa makusudi wa kuadhimisha kwa ubaguzi Waafrika waliokufa.¹⁰⁵

Majina ya waliokufa yalikuwa yanajulikana na Tume lakini sio mahali pa kuzikwa; maadhimisho juu ya kumbukumbu yalikuwa kwa mujibu wa nambari tu, na majina yalihifadhiwa katika usajili wa kumbukumbu.

Mifano ya aina hii inaweza kuonekana kwenye kumbukumbu zilizojengwa kwa ajili ya Jeshi la India nchini Misri, Afrika ya Mashariki na Irak, na kumbukumbu zilozengwa kwa wale Waafrika wengineo nchini Nigeria na Sierra Leone. Katika kesi za awali, uamuzi wa kutojumuisha majina ulitokana na masuala kadhaa yaliyounganika lakini kimsingi yalitokana na kuokoa gharama kwa upande wa mamlaka ya koloni la Uingereza la India, kwa kukosa kumbukumbu za kuridhisha na kwa imani kwamba maeneo haya kamwe hayatatembelewa na waombolezaji wa kihindi. Katika kesi ya wale waliokufa Afrika

¹⁰⁴ CWGC/1/1/7/E/63, 'Mkurugenzi wa Kazi za Browne kuhusu maadhimishi ya mazishi nchini Nigeria na Gold Coast', 12 Juni 1930, p. 371; kwa orodha ya majina ya wale waliozikwa katika makaburi ya Lagos Ikoyi, angalia Ripoti za Usajili wa Makaburi katika CWGC/1/1/7/E/63, pp. 63–5; Ikiwa ni pamoja na yale yaliyotajwa, jumla ya makaburi 72 ya 'wenyeji' yalikuwa bado yameorodheshwa katika ripoti ya Nigeria, yalienea katika makaburi 11, angalia CWGC/1/1/7/E/62, 'Muhtasari wa Makaburi', pp. 96–8.

¹⁰⁵ CWGC/1/1/7/E/53, 'Barua: Fabian Ware kwa J.N. Cormack', 23 Juni 1922, pp. 35–6.

Magharibi, uamuzi ulitokana zaidi na mamlaka ya kikoloni katika dhana yao ya 'ukosefu wa ustaarabu' au kutokuona umuhimu miongoni mwa wapagazi waliotengwa.

Mnamo Oktoba 1925, Mkurugenzi wa IWGC wa Rekodi alimwandikia Katibu Mkuu Msaidizi akieleza wazi sera ya Tume kuhusu maadhimisho ya waajiriwa wa India, ambao wangechukuliwa sawa na askari wa Kiingereza barani Ulaya, Gallipoli, Somaliland na India. Hata hivyo, nchini Misri, Palestina, Syria, Irak na Afrika Mashariki (isipokuwa Dar es Salaam), makaburi ya Wahindi yalitakiwa kuwekewa alama ya kumbukumbu za uwakilishi, wakati makaburi ya kandokando na ya wale waliokosekana yangeadhimishwa kwa namba juu ya kumbukumbu.¹⁰⁶ Sera hizi zinaweza kuonekana kihalisi kwenye kumbukumbu ya awali ya Port Tewfik, ambayo iliadhimisha siku ya wahindi 4,000 waliokufa. Hii ilitokana na kampeni nchini Misri na Palestina ambapo hawakuwa na kaburi lililotambulikana. Mwanzoni mwa miaka ya 1920 inaonekana IWGC ilifanya kazi kwa dhana kwamba majina ya askari hawa yangeandikwa, hata hivyo, ilipotangazwa rasmi mwaka 1926, majina yalionekana tu katika kumbukumbu za usajili – kumbukumbu za usajili zilibeba idadi tu ya majina ya wafu na nyadhifa zao katika vikosi vyao.¹⁰⁷

Takribani wakati huo huo serikali ya India pia ilihusika katika mazungumzo kuhusu kumbukumbu zilizokosekana huko Gallipoli, Afrika Mashariki na Mesopotamia, ambapo hatimaye ilikubaliana na ujenzi wa makaburi ya pamoja ya Waingereza na Wahindi. Kutokana na sababu za kiuchumi zilizoonekana na utawala wa Uingereza na India, kumbukumbu hizi za pamoja ziliahidi kupunguza mzigo wa fedha zao. Kutokana na majadiliano yaliyoendelea kwengine, IWGC ilihoji kama kumbukumbu hizi zitajumuisha majina ya waliokosekana au taarifa za ujumla kuhusu idadi na vikosi. Kwa kujibu, Jenerali Cobbe wa Ofisi ya India papo hapo hakuwa na furaha jinsi hali hii ingelijitokeza. Yenyewe itakuwa 'vibaya kama kumbukumbu kama hizo zitakuwa na majina binafsi kwa

¹⁰⁶ CWGC/1/1/9/D/29, 'Mkurugenzi wa Rekodi kwa Arthur Browne kuhusu kumbukumbu za Wahindi na askari wengine Wenyeji', 20 Oktoba 1925, pp. 35–6.

¹⁰⁷ Arthur Browne aliibua swali la majina ya watu binafsi katika CWGC/1/1/9/D/12, 'Barua: Browne kwa Kanali Chitty, Ofisi ya India', 17 Desemba 1921, p. 59. Mnamo Septemba 1922 iligunduliwa na Browne kwamba Serikali ya India na Ofisi ya India 'kufuatana na sababu anuwai waliamua kwamba majina ya askari binafsi wa India hayapaswi kujumuishwa kwenye Ukumbusho, lakini tu majina ya vitengo' - CWGC/1/1/79/D/12, 'Barua: Browne kwa Kanali Chitty', 7 September 1922, pp. 139–140.

Waingereza waliokosekana na majina ya Vitengo tu kwa Wahindi na idadi ya wahindi waliokosekana'.¹⁰⁸ Walakini, kabla ya 2003, Ukumbusho wa Waingereza na Wahindi huko Dar es Salaam na Nairobi walipeleka majina ya Kihindi kwenye sajili za kumbukumbu.

Labda muhimu zaidi ya yote katika mahesabu haya ni Kumbukumbu ya Basra. Hii ni moja miongoni mwa kumbukumbu kubwa kwa wale waliopotea, ambayo ilijengwa na Tume baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Inaadhimisha zaidi ya wapiganaji 40,600 wa Himaya ya Uingereza, wengi wao ni Wahindi, ambao hawana makaburi yanayojulikana. Ingawa mara nyingi imekuwa ikidhaniwa kuwa hii ilitokana na asili ya mapigano – askari wakiwa medani, katika maeneo yaliyotengwa na wakati mwingine bila mafanikio - sababu kubwa ambayo Wahindi wengi hawakutambulikana ni uamuzi uliochukuliwa na Wasimamizi Wakuu wa jeshi la India mwaka 1918. Kwa kuwa makaburi mengi ya Wahindi hayakuwekewa alama vizuri katika medani za vita, na kwa sababu kuchomwa moto kwa waliokufa hakukusajiliwa ipasavyo na Jeshi la India kwenye uwanja wa mapambano, Vitengo vya Usajili vya Makaburi ya DGRE viliagizwa kulenga juhudi zao hususan kwenye mazishi ya Waingereza. Uhaba wa mafuta kupita maeneo mbele zaidi ya Basra ulimaanisha pia wote waliokuwa wamekufa walikuwa wamezikwa kufuatana na jinsi kampeni ya vita ilivyoziidi kuendelea. Na kushindwa kuweka alama za makaburi ilimaanisha kuwa kuchomwa kwa wale waliokufa zamani hakukuweza kufanyika bila kuhatarisha miili ya wale ambao jambo kama hili halikuwa sahihi. Matokeo yake, idadi ndogo sana ya makaburi yaliyowekewa alama yalinusurika nchini Irak, wakati vifo vingi vilivyobakia vya Wahindi vilionyeshwa kama majeruhi waliopotea.

Ilikuwa ni sababu ya askari hawa ndo kumbukumbu ya Basra ilijengwa. Lakini ilijengwa kwa shinikizo kutokana na kutokuwa na uhakika wa nafasi ya Uingereza nchini humo. Kwa hakika, kutokana na masuala ya ndani ya kisiasa na hatari za kuendelea kufanya kazi huko, IWGC ilitaka kumbukumbu ijengwe kwa haraka, vinginevyo ilihofiwa kamwe haitakamilika.¹⁰⁹ Hata hivyo, matatizo yaliibuka haraka kutokana na orodha ya waliopotea, ambapo wakati ilipopatikana kwa urahisi kwa usajili wa vikosi vya Kiingereza

¹⁰⁸ CWGC/1/1/9/D/12, 'Barua: A.S. Cobbe to Arthur Browne', 29 Septemba 1922, p. 141.

¹⁰⁹ CWGC/1/1/7/E/77, 'Mhadhara umetolewa na Kanali Durham (Mkurugenzi wa Kazi)', 5 Mei 1924, pp. 14, 38.

na kwa maafisa wa Kiingereza, katika vikosi vya Wahindi iligundulika kuwa orodha haikukamilika na haiendani na tahajia ya majina na maelezo mengineyo kuhusu ngazi za vyeo vya Wahindi. Nchini Ufaransa, IWGC ilikuwa imekabiliwa na shida kama hizo za kukusanya orodha sahihi ya wapiganaji waliokosekana wa Kihindi kwa ajili ya kumbukumbu za Neuve Chapelle, japo idadi iliyobidi kusahihishwa - 4,600 ikilinganishwa na 30,000 - ilikuwa tofauti sana. Katika kutafuta suluhisho la haraka linalokubalika, IWGC iliishauri Mamlaka ya India na kuipa ufumbuzi wa aina tatu unaowezekana kutatua tatizo hili:

- Kujenga kumbukumbu moja kwa ajili ya Waingereza waliokosekana na kumbukumbu nyingine kwa Wahindi wakati orodha ikipatikana na hali ya hewa ya kisiasa kuboreshwa.
- Kujenga kumbukumbu na kuwepo kwa nafasi ya majina ya askari wa Kihindi, ambayo ingeongezwa baadaye.
- Kuadhimisha askari wa Kihindi kwa nambari.

Katika mkutano wa baadaye na Katibu wa Jeshi wa mamlaka ya India pamoja na msaidizi wake, uamuzi wa muda ulifikiwa ili kutatua masuala haya ambapo kumbukumbu zote kwa Wahindi waliokosekana nje ya Ulaya zingekuwa na majina tu ya vikosi vyao husika 'ikifuatiliwa kwa kila mmoja na majina ya Maafisa wa Kiingereza (na wasio na nyadhifa za kijeshi kama wapo), majina ya askari wa kienyeji wasiokuwa na nyadhifa na wengineo.¹¹⁰ Ingawa majina hayangewekwa kwenye kumbukumbu, serikali ya India ilisisitiza kwamba majina yanapaswa kuonekana katika usajili wa kumbukumbu pamoja na usajili wa makaburini katika kesi zote. Kwa hivyo, ilipozinduliwa tarehe 27 Machi 1929, kumbukumbu ya Basra ilionekana kama ilivyokuwa kwenye makubaliano. Majina ya askari wa kawaida wasiokuwa na nyadhifa yaliadhimishwa mmoja mmoja, pamoja na yale yote yaliyoadhimishwa mahali pengine nchini Irak, kwa sasa yanaonyeshwa katika usajili wa kumbukumbu mbili katika makao makuu ya CWGC huko Maidenhead.

¹¹⁰ Waziri wa Jeshi alikuwa Jenerali Bwana Alexander Cobbe na msaidizi wake alikuwa Kanali Walter Willis Chitty, wote maafisa wa Jeshi la India waliotumikia kwa muda mrefu ambao walitoa huduma kubwa huko Mesopotamia wakati wa vita. CWGC/1/1/9/C/26, 'Barua: Lord Arthur Browne kwa Naibu Waziri wa Nchi, Idara ya Jeshi, Ofisi ya India', 14 Machi 1924.

Zaidi ya matatizo ya kijumla yaliyohusika na tahajia na usahihi wa majina ya wanajeshi wa Kihindi na ukosefu wa habari kuhusu maeneo yao walikofia, maamuzi yaliyoashiria jitihada za IWGC kuhusiana na Wahindi waliokufa yanaashiria kupunguzwa kwa gharama kulihusika. Jinsi ambavyo serikali zilizochangia kuifadhili Tume zilitokana na hesabu ya msingi ya idadi ya makaburi iliyoyahifadhi kuambatana na kila mfadhili. Kisha takwimu hii iligeuzwa kuwa asilimia ya bajeti yote, ambayo kwa upande wake ilitumika kupatikana kwa takwimu kwa wale walioadhimishwa kwenye kumbukumbu. Kwa matokeo haya, kwa kuweka alama ya makaburi 5,556 tu, mchango wa serikali ya India uliwekwa kwa asilimia 1.02 tu ya bajeti yote.¹¹¹ Ingawa haizingatii idadi kubwa ya askari wa Kihindi ambao hata hivyo wangechomwa moto na kuadhimishwa kwenye kumbukumbu, athari za kuokoa gharama kwa ajili ya maadhimisho ya kumbukumbu zingeweza kuwa kubwa. Ingawa haiwezi katika hatua hii kuonyeshwa, maadhimisho kwa nambari peke yake kwenye maeneo ya kumbukumbu huenda yangeonekana kuwa nafuu bado. Kwa hivyo, ilikuwa ni mzigo mdogo kifedha kwa utawala wa India chini ya Uingereza kutangaza waajiri wake waliokosekana, hususan kama vile wangeadhimishwa kiidadi kwenye kumbukumbu za pamoja za India na Uingereza.

Huko Afrika Magharibi, Tume ilijenga minara ya kumbukumbu nchini Sierra Leone (Freetown) na Nigeria (Lagos), ambayo ilijumuisha majina ndani ya daftari la kumbukumbu lakini sio kwenye minara yenyewe ya kumbukumbu. Nchini Nigeria hii ilikuwa ni amri ya Gavana, wakati nchini Sierra Leone, hii iliongozwa na wahusika ndani ya Tume.¹¹² Ingawa maandishi ya kumbukumbu ya Lagos yaliorodhesha majina ya vikosi tu, kumbukumbu za Freetown zilikuwa za kuchagua zaidi, kwani majina ya askari 229 na wahandisi yaliandikwa humo, lakini majina ya wapagazi 795 hayakuwekwa. Hata hivyo tofauti na Basra, uteuzi wa kubagua huu haukuwa ni matokeo ya kumbukumbu isiyoy

¹¹¹ Iliamuliwa katika Kongamano la Vita vya Himaya mnamo 1918 kwamba malipo kwa IWGC 'yangeshughulikiwa na Serikali husika kulingana na idadi ya makaburi ya Wafu wao.' Asilimia hizi, na jumla ya pesa zilizotolewa, ziliwekwa katika kila ripoti ya kila mwaka iliyotolewa na IWGC. CWGC/1/1/9/D/12, 'Barua: Mdhambi & Mshauri wa Fedha kwa Browne', 4 Agosti 1922, p. 133.

¹¹² CWGC/1/1/7/E/63, 'Barua: K.L. Hall kwa kaimu Katibu Mkuu wa Serikali ya Nigeria kwa Katibu IWGC', 14 July 1928, pp. 268–9.

sahihi au mahitaji ya ujenzi wa haraka, bali ilihusishwa moja kwa moja na ubaguzi kwamba kuna 'ukosefu wa ustaarabu' miongoni mwa wale waliotengwa.

IWGC ilanza kuzingatia suala la Sierra Leone baada ya kuchelewa sana, kwani ilikuwa hadi Januari 1923 tu wakati Tume ilipokubaliana na kamati ya maeneo husika kuwa wakala wao rasmi nchini.¹¹³ Hapo awali maendeleo yalikuwa yamezorota na taratibu za usajili wa makaburi na upangaji wa mipango ya makaburi, na IWGC kushika uongozi wa haya majukumu yote ilichuchukua miaka mingi. Kufikia mwaka wa 1926 ilikuwa wazi kwamba, ingawa walijua makaburi ambayo wananchi wengi wa Sierra Leoni walikuwa wamezikwa, lakini jinsi mazishi yao yalivyofanyika, makaburi hayakuweza kutambulikana. Kwa kutoa mfano mmoja tu, katika makaburi ya Wilberforce huko Freetown – karibu na maeneo ya kambi kuu la jeshi kikosi cha Afrika Magharibi na eneo la makaburi muhimu la Waafrika – hakukuwa na jitihada yoyote iliyowahi kufanywa kuweka alama makaburini ili kuyatambulisha, na eneo la makaburi yenyewe lilisemekana kuwa katika 'hali mbaya ya kushtusha na ya kutoyajali' Eneo hili la makaburi lilikuwa chini ya mamlaka ya 'Mkuu wa Kijiji cha Wilberforce', na afisa mkuu wa kikosi mwenye amri aliamini hali hii iliakisi ukweli kwamba, 'uwekaji wa mawe ya makaburi...hauna maana wala haumridhishi askari wa Afrika Magharibi'.¹¹⁴

Kufikia 1927 afisa huyo huyo mwenye amri, Luteni-Kanali A.E. Norton, alianza kuweka shinikizo la ujenzi wa kumbukumbu kuu kwa vile aliamini kitengo chake na watu wake hawakupata kutambulika vya kutosha.¹¹⁵ Kutokana na matatizo ya kuweka alama za makaburi na madai ya ukosefu wa shauku katika taratibu hizo kutoka kwa wenyeji, na pia

¹¹³ Kamati hii ilianzishwa mnamo Julai 1922, chanzo chake ni waraka kutoka Ofisi ya Ukoloni ya Juni 1921 kuhusu jukumu la IWGC, tazama CWGC/1/1/7/E/68, 'Rekodi ya Kamati ya kuchunguza na kuripoti juu ya makaburi nchini Sierra Leone', 26 Julai 1922, pp. 39–42; juu ya kuwa wakala wa IWGC nchini Sierra Leone, tazama CWGC/1/1/7/E/68, 'Barua: Browne kwa Katibu wa Ukoloni Sierra Leone', 24 Januari 1923, pp. 62–5. Kama sehemu ya uanachama wake, nahodha wa Kikosi cha Afrika Magharibi aliteuliwa kusaidia katika maswala yanayohusiana na makaburi ya wanajeshi wa Afrika Magharibi.

¹¹⁴ CWGC/1/1/7/E/68, 'Wakala wa Ndani ya Nchi Sierra Leone kwa Katibu wa IWGC London', 14 Juni 1926, pp. 92–3; CWGC/1/1/7/E/68, 'Vidokezo vya Mkutano wa Browne na Luteni-Kol. A.E. Norton (kamanda Kikosi cha Afrika Magharibi)', 28 Julai 1926, p. 99; CWGC/1/1/7/E/68, 'Barua: Norton kwa Katibu wa Wakala wa IWGC Ndani ya Nchi ya Sierra Leone', 24 Mei 1927, pp. 116–18.

¹¹⁵ Kikosi cha Afrika Magharibi hakikuwa sehemu ya Vikosi vya Mbele vya Afrika Magharibi. Kilikuwa kitengo cha kawaida ambacho kilitangulia WAFF, na makao yake makuu yako Freetown.

yale makaburi ya Waafrika yaliyopo huko Wilberforce kupata wageni kwa nadra tu, alishauri kujenga kumbukumbu katika eneo la wazi lililotengwa kwa mapumziko ya watu. Tofauti na Afrika Mashariki, imeonekana kumekuwa na hisia kali za wenyeji – hasa kutoka kwa maafisa wa vikosi – majina yalitakiwa kutoa utambuzi sahihi kwa mihanga iliyotolewa. Kama rais wa shirika la wenyeji alivyosema, 'sasa ni zaidi ya miaka minane tangu kusitishwa kwa Vita...lakini bado hadi wakati huu hakuna kumbukumbu yoyote ambayo imejengwa katika koloni hili kwa wale Waafrika waliojitolea maisha yao...katika pale ambapo ni nyumbani kwao wenyewe'.¹¹⁶ Wakala wa Sierra Leone na IWGC hatimaye waliidhinisha wazo la kumbukumbu kuu huko Freetown na kukubali kwamba makaburi yoyote yasiyokuwa ya Wazungu yataruhusiwa kurudia hali ya kiasili. Hata hivyo, ilipofika kwenye swali la majina yatayojumuishwa kwenye kumbukumbu, Browne na Mkurugenzi wa Kumbukumbu, Henry Chettle, walikubali kwamba askari walikuwa wamechukuliwa kuwa wana uwezo lakini kwamba wapagazi hawakuwa na 'ustaarabu wa kutosha kuhalalisha kujumuishwa'.¹¹⁷ Kwa kawaida, kutokana na idadi yao kubwa sana, pia ilikuwa gharama nafuu na rahisi sana kujumuisha majina ya wapagazi katika kitabu cha usajili badala ya kumbukumbu yenyewe.

Takwimu za mwisho za Kumbukumbu ya Freetown zinajumuisha nyadhifa nyingine 61 za Kikosi cha Afrika Magharibi, pia askari 55 wa Kikosi cha Sierra Leone cha Ulinzi wa Mipaka ya Afrika Magharibi na Wahandisi wa Royal 113 (Usafiri wa Majini); na kuondoa majina ya wananchi 795 wa Sierra Leone waliokufa wakati wakifanya kazi kama wapagazi wakati wa vita, ambao badala yake walikumbukwa kwa nambari pekee. Hatima hii hii iliwakumba watu wawili wa Usafiri wa Majini na watatu wa Kikundi cha Watabibu wa Sierra Leone ambao walikuwa wamefariki dunia ikiwa ni sehemu ya kikundi kinachoelekea Mesopotamia ambayo iliungwa mkono na Dar es Salaam kwa kutumika kama wapagazi. Ingawa Chettle alipendekeza kujumuisha majina haya matano kwenye kumbukumbu kutokana na vitengo vyao vya awali, mamlaka za Sierra Leoni zilisema hivi sasa wao

¹¹⁶ CWGC/1/1/7/E/68, 'Barua: Wakala wa Ndani ya Nchi Sierra Leone kwa Katibu wa IWGC London', 25 Mei 1927, pp. 113–15.

¹¹⁷ CWGC/1/1/7/E/68, 'Browne kwa Mkurugenzi wa Rekodi', 17 Septemba 1927, p. 131; CWGC/1/1/7/E/68, 'Mkurugenzi wa Rekodi kwa Browne', 29 Oktoba 1927, p. 134; CWGC/1/1/7/E/68, 'Barua: Browne kwa Fabian Ware kuhusu Sierra Leone', 17 Novemba 1927, pp. 139–40.

washapangiwa kuwa kama wapagazi.¹¹⁸ Maadhimisho haya kwa idadi yalibaki hadi baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, wakati muundo wa ujenzi wa bango la kumbukumbu lilipobadilishwa ili kuwezesha kujumuisha idadi kubwa ya askari waliokufa kutokana na vita hivyo. Vifo vyote vya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia vilienea kwenye ujenzi wa bango moja na taarifa zote kuhusu Wapagazi wa Sierra Leone ziliondolewa, (na sasa zipo kwenye hifadhidata ya majeruhi). Ingawa hawa wapagazi 'wamepangiwa' kwenye kumbukumbu za hifadhidata ya majeruhi, bado hawapo kwenye kumbukumbu yenyewe.

Hatimaye, majina 952 ambayo awali yaliachwa kwenye kumbukumbu ya Lagos sasa yamewekwa kwenye kumbukumbu iliyobadilishwa jina na kugeuzwa upya kuwa kumbukumbu ya Abuja, iliyokamilika mwaka 2016. Wakati hii haiondoi athari za maamuzi hayo ya zamani, inaleta usawa katika maadhimismo yanayotarajiwa leo. Uamuzi kuhusu mahali pa kuyaandika majina ya wapagazi wa Sierra Leone na wale wanaokosekana kutoka Kumbukumbu ya Basra bado haujafanywa.

Majina ya watu waliokufa na maeneo ya maziko hayakujulikana na Tume, hivyo iliamuliwa kuadhimishwa kwa kumbukumbu za kijumla, zisizokuwa na majina ya wahusika.

Ufutaji muhimu wa tarakimu kutoka kwenye hifadhidata na kumbukumbu za CWGC ni zile ambazo shirika halijawahi kupata maelezo yake - wala majina yao wala maeneo yao ya mazishi. Hili linajulikana kuwa suala muhimu sana kote Afrika Mashariki na Misri. Vita barani Afrika vilipiganwa sana dhidi ya hali ya hewa na ardhi, kama ilivyokuwa adui, huku usafiri ukiwa moja ya vikwazo vikubwa mno. Bila barabara za lami na kuwepo kwa magonjwa ya nchi za joto yakileta ugumu kwenye shughuli ya kuwaweka wanyama wawe hai, palitokea mahitaji yasiyo na kikomo kwa wapagazi kuwalisha wanajeshi ili waendeleo kupigana. Kama matokeo, inakadiriwa kuwa karibu wanajeshi 50,000 wa Kiafrika na zaidi ya wafuasi milioni moja wa Kiafrika (wafanyakazi, wabebaji au wapagazi) walikuwa katika kazi za Uingereza na ukoloni. Kama ilivyoainishwa mapema, kwa uchache kiasi cha

¹¹⁸ CWGC/1/1/7/E/68, 'Mkurugenzi wa Rekodi kwa Waziri wa Koloni Sierra Leone', 4 Oktoba 1929, p. 222; CWGC/1/1/7/E/68, 'Sierra Leone Colonial Secretary to Director of Records', 8 January 1930, p. 256.

100,000 na uwezekano wa hadi 300,000 walikufa kutokana na kufanya kazi kupita kiasi, utapiamlo, na magonjwa.¹¹⁹

Wengi wa watu hawa walilelewa ndani ya nchi, mara nyingi kwa njia ya viwango tofauti vya kulazimishwa. Kumekuwa na ubishani kwamba ukosefu huu wa utaratibu maalum umezuwua kukamilisha taarifa husika kwenye maandishi, maana ni vigumu kutabiri ni wangapi hatimaye walitoa huduma kama vile kushindwa kutabiri ni wangapi waliangamia. Katika miaka ya 1920, kwa kuzingatia taarifa zilizopo, IWGC ilifanya kazi kwa dhana kwamba takribani wanajeshi 5,000 wa Kiafrika na kati ya wapagazi 40,000-50,000 walikuwa wamefariki dunia na ilikuwa inahitajika maadhimisho huko Afrika Mashariki. Hata hivyo, katika takribani kesi zote hawakujua majina yao au maeneo ya mazishi, na inaonekana kwamba hakuna tarakimu kamili au hata sehemu ya tarakimu iliyowahi kutumwa, au kutafutwa kikamilifu na IWGC.¹²⁰ Katika ripoti ya Kitengo cha Usajili wa Makaburi ya Afrika Mashariki ya Desemba 1919 ilielezwa kuwa, licha ya idadi kubwa inayokadiriwa kuwa tayari imetolewa, kulikuwa na 'makaburi yaliyotambuliwa' kwa Wazungu 2,729, vikosi 322 vya Wahindi na vikosi 350 vya Waafrika - hakuna kumbukumbu yoyote iliyofanywa kwa wapagazi au waajiri wengine wasio wapiganaji. Ripoti hii, pamoja na nyengine nyingi, pia ilibainisha kuwa 'ilikuwa nadra sana kupata makaburi ya Wanajeshi wenyeji waliowekeka alama ya vitambulisho vya baadaye na hii pia inawahusu Wanajeshi wa Kihindi'.¹²¹

¹¹⁹ Tazama kwa mfano Hodges, 'African Manpower Statistics', p. 116; Killingray, David, 'Repercussions of World War I in the Gold Coast', *Journal of African History*, Vol. xix, Na. 1 (1978), pp. 39-56; Killingray and Matthews, 'Beasts of Burden', pp. 17-18; Pesek, Michael, 'The war of legs. Transport and infrastructure in the East African Campaign of the First World War', *Transfers*, Vol. 5, No. 2 (2015), pp. 110-13; Paice, Edward, *Tip and Run - the Untold Tragedy of the Great War in Africa* (London: Weidenfield & Nicolson, 2007), pp. 392-3; Strachan, Hew, *The First World War in Africa* (Oxford: Oxford University Press, 2004), p. 3.

¹²⁰ Tazama, kwa mfano, CWGC/2/2/1/88, *Mkutano wa Tume Na.88*, 12 Mei 1926, pp. 8-11; Kulingana na Killingray na Matthews, orodha ya majina ya wapagazi wa Afrika Magharibi iliyotumwa Afrika Mashariki, au 'Kitabu Chekundu', kilipotea mahali fulani kati ya Afrika Mashariki, Afrika Magharibi na Uingereza. Tazama Killingray na Matthews, 'Beasts of Burden', p. 21.

¹²¹ CWGC/1/1/7/E/52, 'Kumbukumbu ya Makaburu yaliyopatikana, yasiyopatikana na yasiyo na alama na Capt. G.B. James, Ag. OC GRU, kwa Mkurugenzi, DGRE London', 11 Desemba 1919, p. 57.

Mnamo Januari 1920, George Evans, kabla ya kuanza kazi yake na Tume, aliiandikia IWGC kusema kwamba wakati baadhi ya watu 50,000 wa Jeshi la Askari Waajiriwa walikuwa wamefariki, hakuna alama za utambulisho zilizowahi kuwekwa kwenye makaburi yao. Pia alibainisha kuwa 'wengi wa wenyeji ambao wamekufa ni wale wenye asili ya nusu ushenzi na hivyo 'ujenzi wa kusimamisha jiwe katibu kaburi la binafsi ni kupoteza fedha za umma'. Hata hivyo, alipendekeza kwamba wale wanajeshi Wakihindi na Wakiafrika ambao walikuwa wamezikwa katika 'makaburi halisi katika Vituo mbalimbali vya kijeshi' wanapaswa kuwekwa mawe binafsi kwenye makaburi yao. Kwa 'wale waliozikwa vichakani, kama ilivyo kwa wapagazi', hata hivyo, Evans alifikiria kwamba 'aina fulani ya Mnara unaoonyesha askari wa Kihindi, Askari wa Kiafrika na Mpagazi ingetosha.¹²² Wakati maoni kama hayo na lugha inayotumika kuyaelezea yanakwenda kinyume na kanuni za msingi wa IWGC, ilikuwa ni mazingatio ya vitendo yanayodaiwa kuwa yaliyoshinda. Hii iliimarishwa na mawasiliano na ofisi ya Mamlaka ya Ukoloni mwaka 1927, iliyosema kwamba utaratibu wa kuita jina moja moja kwa vifo vya 'wenyeji' haijawahi kuwepo Afrika Mashariki.¹²³ Wakiwa wamepata nguvu kwa sababu hizi, Tume ilipata kisingizio cha urahisi cha uamuzi wake wa kusimamisha kumbukumbu za uwakilishi, zisizo na jina kwa Waafrika waliokufa. Akitafakari juu ya hili, mrithi wa Evans, J.N. Cormack, alisema:

Hakuna ulinganisho dhahiri ambao unaweza...kulinganishwa kati ya utukuzaji unaopewa na Tume ya Makaburi ya Vita vya Himaya, kwa Majeshi ya India na Afrika kwenye maeneo yaliyokuwa nyuma kimaendeleo na yaliyosambaa kote Afrika Mashariki, ambamo hali ya vita imefanya kitambulisho cha mtu binafsi hasa kwa mataifa hayo, kutowezekana kabisa, isipokuwa katika idadi ndogo sana ya watu.¹²⁴

Wakati utafiti unaounga mkono ripoti hii bado haujapata ushahidi wa uhakika kwa madai kwamba majina haya hayakuweza kupatikana, inaaminika kuwa tarakimu kwa angalau

¹²² CWGC/1/1/7/E/52, 'Meja George Evans, OC GRU Afrika ya Mashariki, kwa Mkurugenzi wa Kazi wa IWGC', 31 Januari 1920, pp. 73-4.

¹²³ CWGC/1/1/9/D/29, 'Barua: Bwana Charles Strachey (Ofisi ya Ukoloni) kwa Arthur Browne', 12 Julai 1927, pp. 69-72

¹²⁴ CWGC/1/1/7/E/56, 'Kumbukumbu na J.N. Cormack kwa Mdhambi na Mshauri wa Fedha', 2 Mei 1922, pp. 57-62.

baadhi ya mamia ya maelfu ya watu waliokufa wakiwa wakitoa huduma za upagazi lazima zilikuwepo. Angalau kwa kiasi fulani, imani hii inatokana na utetezi wa Luteni-Kanali Oscar Watkins kuhusiana na fidia ya upagazi baada ya vita, pamoja na ripoti ya kutafakari ambayo iliainisha kuwepo kwa orodha za kina za waliokufa.¹²⁵ Ni mapendekezo yenye nguvu ya Kamati hii kwamba CWGC itatafuta ushahidi wa aina hii mara tu hali itaporuhusu.

Mfano kama huo ulishuhudiwa nchini Misri kufuatia kupotea kwa waajiriwa kati ya 16,000 na 50,000 wa Kikundi cha Wafanyakazi wa Misri na Kikundi cha Wafanyakazi wa Usafirishaji wa Ngamia. Wengi wao hawakuwa na makaburi yenye alama, na IWGC haikupewa orodha ya majina yao. Hivyo, kumbukumbu ya jumla ilipendekezwa tena, ingawa mtindo huo ulitofautiana na ule wa Afrika Mashariki. Kwa hakika, kati ya mwaka 1920 na 1922 mfululizo wa mapendekezo yalitolewa na mamlaka ya Misri kuwaadhimisha wale waliokufa, kuanzia kujenga msikiti hadi kuanzisha mfuko wa udhamini wa elimu.¹²⁶ Hatimaye, katika mkutano wa arubaini na moja wa Tume mnamo Januari 1922, iliishia chaguzi mbili: kujenga shule mbili za msingi huko Port Said na Suez, au kuimarisha maabara ya kumbukumbu iliyounganishwa na Hospitali ya Macho huko Giza. Serikali ya Misri iliunga mkono chaguo la pili, lililogharimu £6,600, na hii iliidhinishwa na kuzinduliwa mwaka 1925.¹²⁷

Licha ya ufumbuzi huu unaoonekana kuwa wenye mantiki kwa tatizo hili lenye changamoto kubwa, kuna ushahidi pia wa wazi unaoonyesha kwamba baadhi ya majina yangeweza kupatikana na IWGC lakini wao walichagua kutofanya hivyo. Katika miaka ya 1920 Tume ilikuwa inafahamu kwamba King's African Rifles (KAR) ilikuwa inajenga kumbukumbu ya vita huko Zomba Nyasaland (sasa Malawi). Pia ilifahamika kwamba inayo majina ya askari zaidi ya 1,200 kutokana na usajili wa kwanza na wa pili

¹²⁵ Ingawa haipunguzi kutoka hatua hii, ni muhimu kutambua kwamba Watkins aliwasiliana moja kwa moja na IWGC kuhusu ujenzi wa kumbukumbu za Afrika Mashariki lakini hakutoa maoni juu ya upatikanaji wa majina. TNA, CO 533/216, 'Ripoti ya Luteni-Kanali O.F. Watkins, Mkurugenzi wa Kazi ya Kijeshi kwa B.E.A. Kikosi cha Utabiri katika kipindi cha Agosti 4, 1914 hadi Septemba 12, 1919', pp. 18-19; CWGC/1/1/9/D/32, 'Kumbukumbu na O. F. Watkins', 9 Oktoba 1924, p. 29.

¹²⁶ CWGC/2/2/1/28, *Mkutano wa Tume Na.28*, 20 Desemba 1920, pp. 3-4; CWGC/2/2/1/36, *Mkutano wa Tume Na.36*, 1921, pp. 3-4.

¹²⁷ CWGC/2/2/1/41, *Mkutano wa Tume Na.41*, 17 Januari 1922, pp 8-9.

yaliyoandikishwa, na kwamba watu hawa hawakuwa katika Kumbukumbu za Usajili wa Tume. Inaonekana kwamba baada ya kuambiwa na Ofisi ya Kikoloni kwamba orodha kamili ya vifo vya KAR haikuwepo Uingereza au Afrika Mashariki, na kwamba orodha ya Zomba iliunda sehemu tu ya majeruhi wote wa KAR, IWGC ilichagua kutooroshesha kile kilichopatikana au kukubali wazo la kujenga kumbukumbu. Kwa kweli, ingawa IWGC ingesema kwamba inaamini kumbukumbu nyingine ambayo imejengwa uwanjani huko Kampala na imetoa maadhimisho ya 'kutosha' kwa Waganda waliokufa, hakuna ushahidi wowote ilikuwa imekubalika.¹²⁸

Utaratibu kama huo ulitokea, japokuwa kwa kiwango kidogo, huko Mwele Ndogo nchini Tanganyika (sasa Tanzania). Hapa IWGC ilikuwa inafahamu sio tu kuhusu makaburi ya pamoja ya watu 14 wa Arab Rifles, ambayo 'iliruhusiwa kurudi katika hali ya kiasili' mwaka 1924, lakini pia kwamba ilijengewa kumbukumbu iliyoingiza majina kwa lugha ya Kiarabu kwa wale waliokufa.¹²⁹ Hata hivyo, wakati Tume ilikiri kuwepo kwake, haikuipitisha, wala haikutoa majina ya kuingizwa katika usajili wake wa wale waliokufa.¹³⁰ Badala yake, ilikubaliwa mwaka 1925 kwamba majina yote ya vifo vya Waarabu kote Afrika Mashariki, (isipokuwa Somalia), vingeadhimishwa kwa kutosha kwa kumbukumbu isiyo na majina huko Mombasa.¹³¹ Utaratibu huu uliendelezwa kote Kenya na katika miaka ya 1920 IWGC ilitahadharishwa kuhusu idadi ndogo ya makaburi ya Waafrika yaliyotambulika ambayo yalikuwa kandokando na Nairobi, lakini ikaagizwa kwamba wafanyakazi hawapaswi 'kuajiriwa kujaribu kufuatilia makaburi ambayo yangeruhusiwa kuendelea kama kawaida yao ya asili'.¹³²

¹²⁸ Tazama faili CWGC/1/1/10/E/14.

¹²⁹ Tazama <https://www.cwgc.org/find-records/find-war-dead/casualty-details/124906/JOHN%20LACHLAN%20MACKINTOSH/#&gid=1&pid=2>.

¹³⁰ Mwaka 2005 kumbukumbu ya Mwele Ndogo ilionekana kuwa nzima kabisa na inatunzwa vizuri.

¹³¹ CWGC/1/1/9/D/29, 'Mkurugenzi wa Rekodi kwa Arthur Browne kuhusu kumbukumbu za Wahindi na Askari Wengine Wenyeji', 20 Oktoba 1925, pp. 35–6.

¹³² CWGC/1/1/7/E/56, 'kumbukumbu: Mahojiano na Vikosi vya OC Troops Koloni la Kenya (Kanali G. Phillips) na Cormack na Rapley', 8 Juni 1922. pp. 99–100; CWGC/1/1/9/D/29, 'Mkurugenzi wa Kazi kwa Mkurugenzi wa Rekodi za Makaburi ya 1/ KAR – Kenya', 25 Februari 1924, p. 6.

Katika tukio tofauti mwaka 1923, Naibu Mkurugenzi wa Ujenzi wa IWGC Afrika Mashariki, J.N. Cormack, alimwandikia Mkurugenzi wa kumbukumbu kusema kwamba alikuwa amekuta 'jalada kubwa lisilokuwa la siri la wale waliorudi' katika Ofisi ya Kumbukumbu za Vita jijini Nairobi. Aliamini hili lingeweza kusaidia kutambua majina na maelezo ya waliokufa. Alisema kwamba 'katika wengi wa waliorejea, taarifa kamili ya wale waliokufa binafsi wenye nyadhifa katika ngazi zote ingeweza kufuatiliwa kwa urahisi (na marudio kuepukwa). Vilevile vikosi vyengine vya Wenyeji kama vile Arab Rifles vingeweza kuchunguzwa'. Hata hivyo, aliendelea, 'Itakuwa jambo la gharama kubwa kuainisha vifo hivi..... na nnadhani kwamba hakuna lengo lolote litakalotekelezwa kwa kuorodhesha majina ya binafsi ya askari wenyenyeji kuambatanisha na nyadhifa, vitengo, tarehe na maeneo ya vifo, nk.'¹³³ Kusita kwa Cormack kutumia fedha kwenye zoezi hili itakuwa imeathiriwa na dhamira ya Tume ya kujenga kumbukumbu zisizo na majina kwa waliokufa, jambo ambalo lilithibitishwa na uteuzi wa msanifu majengo, mwaka mmoja kabla.¹³⁴ Hata hivyo, huu ni mfano usioplingika wa shirika ambalo likijuwa wazi kwa uhakika upotezaji wa fursa kama hii ya kujaza pengo kubwa katika hifadhidata ya waliokufa vitani. Haiwezekani kujua ni majina mangapi ambayo yangeweza kupatikana au kama nyenzo bado zipo. Lakini kuna uwezekano kwamba askari 5,000 wa Kiafrika ambao wanakosekana katika orodha ya mapambano ya Afrika Mashariki ingeweza kuwepo na kutambuliwa. Kinachokuwa wazi ni kwamba watu watano tu wa Arab Rifles wameadhimishwa kwa majina, na wakati zaidi ya 4,200 KAR wanajulikana kwamba walifariki wakati wa vita, ni 401 tu walioadhimishwa kwa jina - zaidi ya nusu ya hao ni maafisa wa Kiingereza wenye nyadhifa, na Maafisa wasiokuwa na nyadhifa.¹³⁵

Mnamo 1924 Arthur Browne alimuomba Rudyard Kipling kutoa maelezo ya kumbukumbu huko Afrika Mashariki. Kama ilivyojulikana 'askari hawa na wafuasi hawakuadhimishwa kibinafsi hata pale ambapo yapo makaburi ya kumbukumbu huwa ni kijumla kwa wote waliokufa'.¹³⁶ Tume ilijenga kumbukumbu hizi kwa sababu haikujua idadi kubwa ya majina na maeneo ya kuzikiwa kwa waliokufa katika uwanja wa mapigano.

¹³³ CWGC/1/1/10/E/14, 'Barua: J.N. Cormack kwa Mkurugenzi wa Rekodi', 20 Desemba 1923.

¹³⁴ CWGC/1/1/9/D/28, 'Barua: Mkurugenzi kwa Kazi kwa Browne', 28 Desemba 1922

¹³⁵ CWGC/1/1/10/E/14, 'Kiwanja 2, Majeruhi wa KAR', 2 Oktoba 1923.

¹³⁶ CWGC/1/1/9/D/32, 'Barua: Browne kwa Rudyard Kipling', 29 Mei 1924, p. 11.

Lakini pia iliwaondolea fursa ya kutilia maanani kukumbukwa kwa watu binafsi ambao hawakuwafahamu na pia wale ambao bado wangeweza kupatikana. Katika karne hii moja iliyopita, kuna uwezekano wa kuwa vigumu zaidi kurekebisha uamuzi huo kuwa sambamba na mamlaka ya awali ya Tume. Hata hivyo, ni msimamo wa Kamati hii kwamba hii haipaswi kuzuia CWGC kuendelea kujaribu kufanya hivyo.

SEHEMU YA 4 – MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

i. Hitimisho

Kwa namna nyingi inaeleweka kwamba shughuli za IWGC wakati wa kufatilia Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia hazikuwa kamilifu. Shirika hilo lilighushiwa katika machafuko ya migogoro na kazi yake ilihusu viwanja vilivyovamiwa wakati wa vita vya dunia. Kazi hiyo ilikuwa mpya, haikuwahi kukabiliwa na yenye dhana iliyo na changamoto nyingi. IWGC ilikuwa ikiandika kitabu cha kanuni jinsi ilivyosonga mbele, si kwa sababu haikuwa na maandalizi au haikuwa na ufanisi, lakini kwa sababu ilikuwa anzilishi. Zaidi ya mwanzo huu wenye changamoto na mapungufu yaliyowekwa kwenye shirika, hata hivyo, ni wazi pia kutokana na ushahidi uliowasilishwa hapa kwamba IWGC ilikuwa na jukumu au ilikula njama katika maamuzi yaliyofanywa nje ya Ulaya ambayo yaliathiri kanuni zake na kuwatendea waliokufa vitani kwa namna tofauti na mara nyingi siyo kwa haki sawa. Sababu zenyewe zilikuwa nyingi na zilitofautiana, na katika kesi chache sana zilifanya hivyo kwa upande mmoja. Hata hivyo, matokeo ya ripoti hii yanakwenda kinyume na maelezo ya kawaida ya historia ya IWGC. Historia hii inahitaji kurekebishwa na kushirikishwa, na kazi ambayo haikukamilishwa tangu miaka ya 1920 inahitaji kuwekwa sawa pale inapowezekana.

Utafiti huu umeonyesha kwamba, mara nyingi, IWGC ilitegemea wengine kutafuta miili ya wafu. Pale ambapo haikuweza kuwapata, ilifanya kazi na ofisi za nchi kutengeneza orodha za wale ambao hawakurudi na kubaki kama wasioelezeka. Kutokana na shinikizo na mkanganyiko uliosababishwa na vita hivyo, kwa njia nyingi haishangazi kwamba makosa yalifanywa katika hatua zote mbili. Kinachoshangaza, hata hivyo, ni idadi ya makosa - idadi ya majeruhi walioadhimishwa bila usawa, idadi iliyoadhimishwa bila majina na idadi nyenginezo ambazo hazikujulikana kabisa. Wakati mwengine IWGC ilikuwa na uwezo mdogo wa kufanya lolote: bila miili wala majina, kumbukumbu zao za jumla zilikuwa ni njia pekee ambayo baadhi ya makundi yangeweza kuadhimishwa wakati huo. Hata hivyo, kuna mifano ambapo shirika pia lilipuuza kwa makusudi ushahidi ambao huenda ungeweza kuwaruhusu kuwapa baadhi ya majina hayo. Kwengine, maafisa wa Tume katika miaka ya 1920 walifurahia kufanya kazi na tawala za mitaa kwenye miradi katika Himaya ambayo ilikwenda kinyume na kanuni za usawa katika heshima za kifo.

